Maswali na Majibu Juu ya Waebrania, Sehemu ya I

Angefanyaje bila Mungu? Hilo lingekuwa halisi, sivyo? Halingefanyika bila Bwana.

1 Sitayahubiri hayo yote. Lakini nilidhani ningeshika jambo nzito, mwajua, kwa hivyo heri nijitayarishe. Lakini, ee, ilikuwa rahisi mno. Kwa hivyo labda basi hakuna maswali mengi sana miongoni mwa watu basi, ambayo... Ni... maswali mepesi na rahisi. Vema, nina furaha kujaribu kuyajibu vema niwezavyo, kwa msaada wa Bwana.

2 Na kama Dada Arganbright yumo humu usiku huu... Dada Ruth. Uko humu, Dada Ruth? Pale. Nina ile... Ee, naam nina ile anwani hapa, na... La, sina. Vema, naweza kuipata papa hapa. Nilikuwa nayo katika kijitabu changu, nami nilikiacha nyumbani. Sasa, askari wakinishika nikienda nyumbani, Ndugu Fleeman, njoo unisaidie. Mwambie Billy nime... niliacha kijitabu changu nyumbani, ninaendesha gari bila leseni usiku huu. Nilidhania nilikuwa nayo mfukoni; ndiyo kwanza nibadilishe nguo zangu. Niliingia upesi, jioni hii, nilikuwa nikikata nyasi upesi sana ikanibidi kukoma na kuharakisha na kupewa nguo za kubadilishia na kukimbia hapa, nami nilikuja na ile kamusi, lakini waweza kuipata baadaye toka pale.

3 Usihuzunike juu ya barua *hiyo*. Endapo sijapata kamwe kupata nyingine mbaya kuliko hiyo, hiyo ingekuwa barua nzuri. Hiyo ilikuwa nzuri. Hiyo ilikuwa nzuri mno. Niliwaambia singeisoma, lakini niliipata, mwajua, na singalijizuia tena. Nilishangaa tu yeye alisema nini. Na iliandikwa vizuri, vizuri sana, jinsi mwalimu apaswavyo kuandika. Hiyo ilikuwa ni nzuri nami naifurahia. Na yani—yanipa...

4 Ona, napenda barua za mtu ambaye ange—hagekubaliana nawe. Ona ukiendelea tu daima, hakuna anayetofautiana nawe, unakuwa baridi. Yakupasa utofautiane kidogo kusudi upate kufahamu na kupekua-pekua. Na—na unaingia tu kwa shimo moja usipojihadhari; ndipo una—unapata shida unapofanya hivyo. Yakupasa uzidi kupiga hatua na kumpata mtu anayetofautiana nawe kusudi upate kuchambua manyoya yako mara kwa mara.

5 Kule Afrika niliwapata simba wadogo wawili, nao walikuwa wadogo, karibu *hivi*. Simba wenye madoadoa, wadogo sana; simba mdogo wa kiume simba, mdogo wa kike. Na ninge... walifanana na watoto wa paka, walikuwa wadogo sana

hivyo, wadogo. . .viumbe malidadi sana, huku wakicheza tu. Nilikuwa naenda kuwaleta huku Amerika, nimewaweka kwenye tundu la ndege. Ilikuwa nije nao niliporudi, lakini singeweza kupata cho—cho chote kuwachanjia, dawa yo yote. Na hawangeniruhusu kuwaingiza Marekani bila wao kuchanjwa kwanza, na singeipata katika Afrika nzima. Lakini kama ungetaka kujua kama yeye alikuwa simba au la, mpige kofi kidogo tu. Yeye angenguruma na akujulishe kuwa yeye ni simba, kwa—kwa hivyo hilo linakuonyesha ulipo msimamo wake.

6 Hivyo divyo ikupasavyo kufanya mara kwa mara, mwajua, kuchambua manyoya nyuma, upate kujua. Lakini, naam, hatupatwi na hasira kama simba; tuna—tunapenda tu hilo, ku. . .watu kuuliza maswali kama hayo, Dada Ruth ni mazuri sana, sana kwangu. Ni. . .napenda hayo, ona. . .Ni yale yaliyo machafu kabisa yanayonichukiza. Lakini haya ni. . .hilo lilikuwa nzuri.

7 Sasa tuna baadhi ya maswali mazuri yanayochangamsha, ya kinyumbani. Kuna mhubiri nyuma kule katika chumba cha nyuma hivi sasa, aliniswali, akisema, "Wale manabii wawili wa Ufunuo 11 je, watakuja kabla ya Kunyakuliwa? Au kabla ya Israeli kutwaliwa? Na nini. . ." Sasa, hayo ndiyo maswali ambayo—ambayo—yanakufunga. Lakini maswali rahisi kama hili ni mazuri.

Lakini sasa, kabla hatujaanza na tuinamishe vichwa vyetu tuombe:

8 Baba, inakumbukwa kuwa ulipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili ulikutwa Hekaluni pamoja na waandishi na wataalam, ukihojiana nao kwu Maandiko Nao walikuwa—walishangaa kwa. . .watu wa kale, walioelimishwa vilivyo katika Maandiko, na huku twaona mtoto mdogo mwenye umri upatao miaka kumi na miwili ange-anawashangaza, katika kufafanua Maandiko. Wewe ulikuwa ukifanya kazi ya Baba Yako. Ulimwambia Mama Yako, "Hujui kuwa yanibidi nifanye kazi ya Baba Yangu kufafanua Maandiko katika maana yake ya kiroho."

9 Na sasa twaomba, Bwana, kuwa—kwa kuwa unajua jinsi tulivyo wanyonge na wadhaifu, na jinsi tutendavyo makosa, kuwa utatujia usiku huu katika hali ya Roho Mtakatifu, ukatufafanulia Maandiko. Nakungojea na kukutegemea Wewe. Na kama ningalithubutu kamwe, kwa wakati wo wote, kuweka mawazo yangu au tafsiri nipate kujinufaisha binafsi, kufanya ionekane kama kwamba jinsi nilivyoeleza ndiyo sahihi, funga kinywa changu, Bwana, jinsi unge. . .Ulivyofanya wale simba, walipomjia Danieli. Wewe ungali Mungu yule yule.

10 Na iwe kwamba. . .tunapomtegemea Roho Mtakatifu, na atufunulie mambo haya. Na ndipo Yeye anapoyanena, uyafanye dhahiri sana hata yule aliyeuliza swali aweza kuipokea. Na

kama inajibiwa kinyume cha yale nimeamini daima, basi na moyo wangu pia ufurahi, Bwana, kujua kuwa nimepata kitu fulani kipya, na njia nzuri ya Bwana. Kwa kuwa wewe ulisema, "Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia."

11 Sasa, baada ya masomo haya ya Maandiko, bila shaka ingeamsha mawazo mengi na kadhalika. Nami naomba, Mungu kwamba kwa vile maswali haya yote yaonekana yameulizwa vizuri na kwa unyenyekevu, Roho Mtakatifu kwa unyenyekevu na uzuri na ayajibu. Kwa kuwa tuliomba katika Jina la Yesu, na kwa utukufu wa Mungu, na kwa ajili ya kuhuisha Kanisa Lake. Amina.

12 Kuna mara nyingi nia za uchoyo kwa cho chote, huharibu tu ladha yake yote. Na sasa, maswali yanayohusu Andiko hili yameulizwa.

13 Sasa, nikitoa mlio kama wa nyoka usiku huu, jino langu limeng'olewa. Nami ninapolirudisha, siwezi kuhubiri, ninazungumza pole pole ninapohubiri, na karibu nipige mbinja.

14 Mke wa Billy Granham alisimulia hadithi kuhusu mumewe, kuwa hali mbovu sana aliyowahi kumwona akiwemo, ilikuwa, alipong'olewa jino la mbele. Na akalipoteza, naye alikuwa na kipindi cha Televisheni wakati uo huo, na—na hange. . . Lilikuwa kwenye sahani pamoja na meno mengine ya nyuma. Na aliponena, alipiga mbinja. "Wiii, wiii," kwa mwanya wa jino lake. Naye alisema alijitupa magotini, akiomba na kutokwa na jasho, dakika kumi kabla ya kile kipindi cha televisheni, na mwishowe walilipata ambapo liliangukia toka kwenye suruali ndefu hata kwenye vidole vya viatu vyake. Mmoja wa watumishi alilipata, hilo jino bandia. Na mke wa Graham akatoboa hiyo siri, humu. Na kwa hivyo nikaipata, kijikaratasi kidogo, nadhani kimo katika Biblia yangu.

15 Na kwa hivyo lina. . .tunapokuwa wazee na wakongwe, mwajua, na hatuna budi kupoteza haya, ni vibaya. Na hivyo basi. . .Nilipokuwa nje kule pamoja na Ndugu Roberson nyuma kule, pamoja nao, nilikuwa nalisugua kwa mswaki asubuhi moja na nikavunja kipande chake, na ilinibidi kulipeleka kwa daktari, ili alirudishe tena. Kwa hivyo Bwana na aongeze baraka Zake.

16 Sasa tunaondoka. . .Nitajaribu kujibu kila moja yayo, nikiweza. Na, Ndugu Tony, kwa neema ya Mungu, nilipata tafsiri ya ndoto yako, na ilikuwa ya ajabu. Nina furaha tele kuona hilo. Na ni tafsiri nzuri, ambapo nadhani haipaswi kutolewa hadharani hapa, kwa hivyo nitakwambia binafsi ikiwa u—usipo. . .ukitaka hivyo. Yeye aliniuliza usiku uliopita, Yeye alikuwa na ndoto, na singalimwambia jinsi ilivyokuwa hadi nilipomwendea Bwana na kuiombea. Ndipo Bwana alinifunulia

na kunipa tafsiri yake. Ni ya ajabu na ni habari njema kwako Ndugu Tony.

17 Sasa, katika swali la kwanza. Naam, sijui nianzie wapi kwanza kwa sababu yote ni mazuri. Lakini sasa tunajaribu tusichukue muda mrefu sana, na labda tunaweza kuyamaliza Jumapili, tusipoyamaliza.

51. Eleza maana ya "adhabu ya milele," katika Mathayo 25:46. "Bali wenye . . ." Hilo ndilo swali.

52. Halafu swali la pili: **"Bali wana wa ufalme watatupwa mbali katika giza la nje," je, hiyo ni sawa na kuwatupilia nje ya mawazo ya Mungu?**

18 Vema, sasa, chukua swali lako la kwanza, linalopatikana katika Mathayo Mt. ishiri . . . sura ya 25 sasa tuta . . . sasa, sijayasoma haya, niliyatazama tu kule nyuma, na nilijitahidi niwezavyo kuyachunguza vizuri nijuavyo—nilivyojua. Na . . . Hebuni tufungue pamoja Biblia zenu, tunaposoma. Sasa, nilitaka kulipata hili toka kwa kamusi ya Kiyunani pia, ili mpate cha—chanzo chake. Nami—na—napenda hilo. Hivyo basi tutakuwa nayo yote—katika zote mbili—Kiyunani na nyinginezo. Na sasa hili litakuwa —litatuchelewesha kwa kusoma kirefu, kwa sababu nitayaendea na kuyafungua Maandiko po pote niwezapo kuyapata, na kuyaweka mahali pao. Vema.

19 Naam, je, kuna mtu ye yote anayetaka Biblia akasome? Kama unaitaka, inua mkono wako. Nasi . . . nadhani tunazo tatu ama nne nyuma hapa. Ukitaka kusoma nasi Maandiko, vema. Ndugu Cox, waweza kuja hapa ukanipa Biblia hizi? Na—ni vizuri kwako ukiweza, ku . . . (kunayo moja, nanyi—mwaweza kuzipeleka chini pale ukitaka, nyingi hivyo). Na ye yote atakaye moja, inua tu mkono wako, kijana huyu atakuletea, ona. Nasi twataka kusoma haya pamoja, na . . .

20 Sasa, kwa kusoma huku na ile sura ya mwisho . . . hizo sura saba za kwanza za Kitabu cha Waebrania. Baada ya kufundisha, bila shaka, wale vijana wanasao haya masomo Ndugu Mercier na Ndugu Goad, wanayo na wanajiandaa kuyachapisha katika kitabu. Nao wanayo. Sasa . . . nasi hata hatujakichambua nusu, tulichambua tu nusu nusu. Nami nadhani wameyachukua hayo kama . . . na wameyachukua yale—yale ya thamani toka kwa yale . . . na kufua tu yaliyo ya thamani, machache tu ya thamani kutoka kwa mafundisho ya ya Waebrania. Ndugu Mercier atakuwa nayo hivi karibuni, ya kishachapishwa, ye yote ayatakaye.

21 Sasa hii humu, huleta . . . Huwezi kumaliza . . . katika kanisa la kinjilisti, ambapo hili kanisa la kiinjilisti. Huwezi kumaliza ma—mafundisho bila kusababisha mashaka na mawazo ya watu wengi. Huna budi. Sasa mimi si mwalimu kamwe, si mfafanuzi wa Biblia kwa vyo vyote vile. Lakini sijaribu kamwe ku—kusema

lo lote, au hata kufanya lo lote, ila kwanza—kwanza kuuliza au kutafuta jambo langu bora zaidi kwake.

22 Niliulizwa na ndugu mpendwa, usiku uliopita, yeye alisema, "Ndugu Branham, Ndugu Seward wakati mmoja alisema kuwa wewe—wewe huwezi ukaingia matatani kamwe. Ona, kuwa kila mara una njia ya kuepukia au kuyatorokea."

23 Nilisema, "Vema, sababu yake, mimi kila wakati hujaribu kufikiria kabla sijafanya cho chote. Ona? Na ndipo watu wakiniuliza, ndipo naweza kuwaambia fikara zangu. Ona?" Lakini ni unapowaza vyema. Na usijafanya cho chote, jaribu kuchukua upande ambao Mungu angependa uchukue, ndipo hakika ingekuwa vigumu kuingizwa shidani.

24 Hungewaza wakati ambao—ambao Ahabu alijaribu kumnasa Eliya. Je, waweza kuwaza ambao Mafarisayo walijaribu kumnasa Yesu? Ona, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa na jibu upesi, kwa sababu kila alichofanya alifanya kwa mapenzi ya Mungu . . . hivyo ndivyo Yeye—Yeye angelipata. Sasa, hivyo ndivyo tunavyotaka kwa hili.

Sasa swali limeulizwa, tutazingatia swali hili:

Eleza maana ya "adhabu ya milele," Mathayo 25:46

25 Sasa sikiza kwa makini. Kila mtu sasa, katika Mathayo 25:46:

> *Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele;*

26 Sasa, swali ni, "Nini . . . Eleza . . . " Sasa neno *milele* latoka kwa neno *daima* na *dawamu,* na *daima* ni "muda fulani." Linamaanisha tu "kiasi fulani cha wakati," kama *daima*. Sasa, kama utasoma. Sijui ni nani walioandika maswali haya, kwa sababu hakuna ye yote aliyeandika jina lake; hawakupaswa kuandika, siyataki, ona.

> Na *hawa watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele;* . . . (sasa tazama, hao ni waovu)

27 Sasa, mtu mpe—mpendwa uliyeuliza swali, hebu soma yaliyosalia.

> . . . *bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*

28 Wao watakwenda katika adhabu ya milele (muda fulani wa wakati), bali wenye haki wana Uzima wa Milele. Hupati kamwe adhabu ya Milele, haiwezekani. Ona, kama wangepata adhabu isiyokoma, wangalikuwa na Uzima wa Milele; wangelikuwa na Uzima wa Milele, wameokoka. Ona, haiwezekani. Sasa ukichunguza, swa—swali lilijiuliza lenyewe . . . linajijibu lenyewe. Ona?

> *Na hao* . . .

> Sasa tazama, nitasoma hapo mbele; . . .

. . .*nao hao* . . .

29 Katika aya ya 20 . . .ya 44:

> . . .ndipo *hao pia* wakajibu, wakisema, *Bwana, ni lini* tutakapoona *njaa* au lini na kiu, *au u mgeni, an uchi* . . . *au u kifungoni tusikuhudumie?*
>
> *Naye—naye atawajibu, akisema, Amina nawaambia,* kadiri *mlivyomtendea* . . .*mmoja wapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea* . . .*mimi.*
>
> *Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya*(daima)*milele:* (hao ni wale waovu) . . .*bali wenye haki watakwenda katika Uzima wa milele.*

30 Ona tofauti? Waovu wana adhabu ya milele, lakini *milele* hapa ni "muda fulani," sasa kama ingelikuwa sawa, ingeliandikwa, "Na hao watakwenda katika adhabu ya milele, wale wengine watakwenda katika uzima wa milele." Ona? Ama, "Wao watakwenda katika adhabu ya Milele, na wengine katika Uzima Dawamu." Ona, kama kuna adhabu ya Milele, kuadhibiwa milele na milele, basi kuna Milele . . .yeye ana Uzima wa Milele; na mna Uzima wa Milele mmoja pekee, na huo hutoka kwa Mungu. Kila kitu kisicho na mwanzo hakina mwisho, kila kitu kilicho na mwanzo kina mwisho. Mwaona kile ninachomaanisha?

31 Sasa, Andiko lenyewe ambalo yule—yule mtu mpendwa alijibu . . .Sasa ukiyatoa kwenye kamusi, *"Na hawa watakwenda katika ainion, kukatiliwa mbali, na katika mile-* . . .*na kwa moto, lile ziwa la moto."* Sasa, neno a-i-n-i-o-n maana yake "muda fulani wa adhabu." Katika kamusi ya Kiyunani, papa hapa "muda wa adhabu," au, "wakati wa adhabu." Ona, "Hao watakwenda katika wakati wa adhabu." Neno lililotumiwa, a-i-n-i-o-n. Ainion, maana yake "wakati, muda, wakati uliokusudiwa." Ndipo lirudishe katika—katika tafsiri hapa, ya Kiingereza, *everlasting* ni "muda fulani wa wakati." Ona, linatoka kwa kiyunani, "muda fulani wa wakati." Neno *ainion*, au *a-i-n-i-o-n, ainion* maana yake ni "muda fulani wa adhabu."

32 Lakini soma nyingine, "Bali hawa wataingia katika Milele." Hiyo ndiyo tofauti. Ona, Uzima wa Milele. Milele yatoka kwa neno Wakati usio na Mwanzo wala Mwisho, na Milele hiyo ni wakati usio na mwanzo wala mwisho. Ni milele *na* milele. Sasa hiyo inapaswa kujibu hilo, ona, kwa sababu ukisoma Maandiko kwa makini sana, utaona.

33 *"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki* . . .*"* Waovu watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele, waadhibiwe kwa muda fulani; labda bilioni moja sijui, lakini bila shaka utaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zako. Lakini kwa hakika kama vile dhambi ilivyokuwa na mwanzo, dhambi ina mwisho. Adhabu ilikuwa na mwanzo, na

adhabu ina mwisho. Na kuzimu kuliumbiwa Ibilisi na malaika zake. Ona? Vema. Sasa, nina lingine chini hapa kujibu hilo, katika dakika chache ambalo ni nzuri, yanaambatana.

> Sasa, Naam, lakini hili hapa: **"Bali wana wa ufalme watatupwa mbali katika giza la nje," hiyo ni sawa na kuwatupa nje ya mawazo ya Mungu?"**

34 La, haingekuwa sawa. Sasa, hapa unarejea kwenye ile Karamu ya Arusi. Sasa, "Na wana wa ufalme," kama ilivyoulizwa hapa. Wana wa ufalme ni Wayahudi, nao walitupwa katika giza la nje. Na wao—wametupwa katika giza la nje, na wamepitia katika wakati wa vilio na maombolezo na kusaga meno. Walitupwa katika giza la nje kwa sababu ingekupea wewe na mimi nafasi ya kutubu, lakini hawakutupwa kamwe nje ya mawazo ya Mungu. Yeye hatasahau kamwe Israeli. Na Israeli ni . . . msomaji ye yote wa Biblia ajua, wanatajwa kama, "wana wa ufalme." Ona, ni ufalme, ile ahadi. Yaani, Mungu anashughulikia taifa, Yeye aliposhughulikia Israeli, ambao ni wana wa ufalme.

35 Sasa, mwakumbuka, Yeye alisema pale, "Na Ibrahimu na Isaka na Yakobo," katika mahali pamoja, "wangekuja na kuketi katika ufalme siku za mwisho. Ona, na kuwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo wangekuwa ufalmeni; wao walikuwano, wao walikuwa watu wa ufalme waliobarikiwa. Bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje.

36 Sasa, mahali marejeo haya yanatokea ni yule—ni yule Bwana arusi. Bwana arusi alipokuja, walipokuwa . . . Wanawali watano walikwenda kumlaki Bwana, na—na wao hawakuchukua Mafuta yo yote katika taa zao. Na wale—wale wengine watano walibeba Mafuta yao katika taa zao. Sasa, ukichunguza, ni mfano mzuri, kwa Wayahudi na Mataifa pia, kama wakataliwa. Kumbuka kuwa kuna *tabaka* tatu za watu kila wakati. Wayahudi, Mataifa (wale wa kidesturi) . . .; Wayahudi, Mataifa, na Kanisa. Ukiyatatanisha hayo, hakika utaingia katika shida ufikiapo Ufunuo. Kwa kuwa usipo . . .

37 Kama Bw. Bohanon alivyoniambia wakati mmoja, alisema, "Billy, mtu ye yote anapojaribu kusoma Ufunuo hupate jinamizi. Naam," yeye alisema "hapa kuna Bibi-arusi chini humu duniani, na wale—na yule joka anatoa maji kinywani mwake kufanya vita pamoja naye." Na alisema, "Ndipo wakati ule ule yule Bibi-arusi amesimama kama wale mia na arobaini na nne elfu," (fundisho la Mashahidi wa Yehova) "kwenye Mlima Sayuni. Na wakati ule ule Bibi-arusi ako Mbinguni." La, la, umekosea.

38 Kuna tabaka tatu za watu. Ona, hao ni, Wayahudi waliokataliwa, na mna wanawali wanaolala ambao maji yale . . . Si Mzao wa mwanamke, ni Wazao waliosalia wa yule mwanamke ambao yule joka alitoa kutoka katika kinywa chake maji . . . Ufunuo 11. Na ndipo, hakika, wale Wayahudi mia na arobaini

na nne elfu hawakuwa yule Bibi-arusi kwa vyo vyote vile, wao ni wazao waliosalia wa kanisa la Kiyahudi. Na fundisho la Mashahidi wa Yehova ambalo huwaweka hao kama Bibi-arusi, sioni jinsi ungefanya hilo, kwa sababu, si Bibi-arusi hao.

39 Ukichunguza pale katika Ufunuo hapo, inasema, "Na wao ni *bikira*, ni *matowashi*." Na towashi alikuwa nini? Wao walikuwa . . . Matowashi walikuwa walinda hekalu waliomlinda malkia, kwa sababu wao walikuwa . . . kwa sab- . . . Wao walikuwa wanaume waliohasiwa. Walikuwa . . . Je, ulitambua, ilisema, "Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake?" Wao walikuwa matowashi wa hekalu. Na lilikuwa kundi lililochaguliwa ambalo Mungu alikuwa amelichagua toka kwa Wayahudi. Sasa, ukichunguza . . . Kama tungepata tu hayo kwa muda mfupi ili lididimie mawazoni mwenu, ambapo hakika mna . . .

40 Hebu tufungue Ufunuo, sura 7, nasi tutaona humu sasa, ambapo . . . ilivyosema. Ni jambo la kupendeza.

> *Baada ya* hayo . . . *nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi* . . . (sasa hii inalingana na Ezekieli 9 ambapo yeye aliona maangamizi ya Wayahudi. Na hapa yeye aona maangamizi ya Mataifa, Ufunuo, sura ya 7) . . . Kisha *nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne (pepo* maana yake "vita na ugomvi") . . . *za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari* . . . *wala juu ya mti wo wote.* (Na hiyo ni vita, "kuzuiliwa")

41 Ee, laiti tungelikuwa na wakati kuliendea kirefu swali hili. Yale yaliyotendeka . . . Hapo ndipo Russel alipotatanishwa. Russel alitabiri, alipoona hayo yakija. Yeye alitabiri "ingekuwa kule kuja kwa Bwana Yesu," bila kujua ilikuwa ni kule—kule kutiwa muhuri kwa Kanisa. Ona?

42 Nao hushangaa jinsi vita vya dunia . . . Vita vya Kwanza vya Dunia. Tazama vilikoma Novemba kumi na moja, saa kumi na moja; mwezi wa kumi na moja, siku ya kumi na moja, saa kumi na moja. Na mara tu baada ya hayo, ubatizo wa maji katika Jina la Yesu ulifunuliwa pamoja na Ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa Kanisa. Hakika, mara tu baada ya hayo.

43 Ukiyapeleka katika Ufunuo, jinsi tulivyoyafungamanisha pamoja, na kati ya Wakati wa Filadelfia na Laodikia. Na Wamethodisti walikuwa na Wakati wa Filadelfia, upendano wa kindugu. Na ule wakati wa kanisa, ulikuwa Wakati wa Laodikia, ambao ni wakati wa uvuguvugu. Na yeye alisema ndani mle, "Nimeweka mlango (mlango uliofunguliwa) mbele yako." Mlango uliofunguliwa! Na ukirejeza Maandiko hayo, yatafungamanisha Ujumbe wote mahali pamoja pale, kuwaonyesheni ninyi ni kamili.

44 Tazama hapa! Kila kitu kilikuwa Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, katika ubatizo, (ambao tutauingilia moja kwa moja) ambalo lilikuwa hakika fundisho la Katoliki na halikuwa kamwe fundisho la Kikristo. La, bwana. Nili. . .Tunalo papa hapa, usiku huu, tutalifikia, tukitumia kamusi, pia. Ona? Naam, bwana, pamoja na historia pia. Hakuna kamwe ye yote aliyewahi kubatizwa hivyo katika Biblia, au kwa miaka mia sita ya kwanza baada ya Biblia. Nami naweza kuthibitisha papa hapa kwa fundisho la Katoliki lenyewe kuwa wao ndio walioanzisha huo, na kunyunyizia na kumwagiana maji.

45 Walitoka hapo wakaingia katika kanisa la ki-Wesley, na kwa kanisa la Methodisti, Methodisti ikaliingiza katika Batisti na Wabatisti wakaliendeleza, na lingali fundihso la uongo! Na naweza kurudi katika Biblia na kuwathibitishia kuwa Biblia ilisema kuwa, "wasema una jina kuwa u hai, nawe, umekufa." Ndivyo hasa. Nao walikuwa. . .

46 Naweza kuthibitisha Biblia ilifundisha ya kwamba wao wangetumia Jina Lake katika ubatizo hadi ule wakati wa giza, kulingana na ule—ule wakati wa nne. . .wa wa—wakati wa kanisa, wakati wa kanisa la Pergamo. Na Yeye alisema. . .Na katika hiyo miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza, kila mtu alisema, "Unayo nuru ndogo iliyobaki, kwa kuwa hujakana Jina Langu."

47 Ilipofikia wakati ule mwingine pale, ule wakati wa Katoliki, Yeye alisema, "Una jina la kuwa 'U hai,' nawe umekufa! Na umelikana Jina Langu." Naam. Ona? Yafungamanisha mfano mmoja mzuri pamoja, Biblia nzima.

48 Sasa chunguza hili:

> . . .*wakizizuia pepo nne*. . .
>
> *Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai:*. . .(ule muhuri)

49 Sasa, muhuri wa Mungu aliye hai ni nini? Sasa, ninyi ndugu Waadventist mtasame, "Adhimisheni siku ya sabato." Nawatakeni mnionyeshe hilo katika Maandiko. Haliko humo. Hamna hata mahali pamoja. . .ambapo—ambapo ule muhuri. . .

50 Ukisoma Waefeso 4:30, upesi sana, utaona Ule Muhuri wa Mungu aishiye ni nini. Waefeso 4:30 yasema, "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi." Si hata mkutano wa ufufuo unaokuja, lakini una usalama wa Milele, (enhee). "Wala msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa Muhuri hata siku ya ukombozi." Tazama kama Waefeso 4:30 haisemi hivyo, ndipo chukueni masomo yenu yaliyo ukingoni mwa karatasi na mfuatilie mengine yote kote Maandikoni mle, na mtaona. Naam, "Kutiwa muhuri hata siku ya ukombozi." Mkiwa na ule Muhuri wa Mungu aliye hai."

51 Sasa, kumbuka, Roho Mtakatifu hakufundishwa kama Ubatizo wa Roho Mtakatifu hata baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Ndiyo kwanza tusherehekee sikukuu ye—yetu ya ukumbusho wa mwaka wa arobaini, miaka arobaini, au sikukuu ya mwaka wa arobaini.

> . . .*akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari.*
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala* mti wo wote, hata *tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu*. . .(sasa unafikia swali lako, *"wale wana,"* ona). . .*watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao* (msidhuru, msiangamize dunia, msiache bomu ya atomiki ilipuke, msikamilishe yote hata watumishi wa Mungu wetu wametiwa muhuri).

52 Sasa, kama tungeyarejeshaa hayo nyuma kule na kuyafuatilia kule nyuma, hata katika kitabu kitwacho *Mwisho wa Vita vya Dunia,* katika kitabu cha pili, wakati Jemedari Allenby alipigana hata akafikia ngome za Yerusalemu, naye alikuwa. . .akampigia simu Mfalme wa Uingereza, na kusema, "Sitaki kuufyatulia risasi mji ule, kwa ajili ya utakatifu wake." Akasema, "Nitafanyaje?"

53 Yeye alisema, "Omba."

54 Naye akaruka juu yake tena, na walipofanya hivyo, wao wakasema, "Allenby yu—yuaja." Na kulikuwako Waislamu ndani mle, walidhani yeye alisema, "Allies wanakuja." Nao wakapandisha bendera nyeupe na kujitolea na Allenby akaingia Yerusalemu na kuitwaa bila kufyatua risasi, kulingana na unabii. Naam, na kuitoa kwa Wayahudi.

55 Ndipo wakamwinua Hitler kuwatesa Wayahudi, na kote ulimwenguni, na kuwarudisha tena kule.

56 Na Biblia ilisema Yeye "angewarudisha tena kwa mabawa ya tai." Nao walipoanza kurudi. . .Gazeti liitwalo *Life* na mengineyo yaliyaandika majuma machache yaliyopita, ambapo waliwarudisha tena maelfu, katika Yerusalemu, nao waliwabeba wazee migongoni mwao. Walihojiwa. Ninayo kwenye ukanda na picha. Na alisema. . .Pale inapepea ile bendera yenye nyota nne ya Daudi ikipepee pale, bendera ya kale sana ulimwenguni, mara ya kwanza ambapo imepeperushwa baada ya miaka elfu mbili.

57 Yesu alisema, "Mtini uanzapo kutoa chipukizi, kizazi hiki hakitapita."

58 Nao ndio hawa wakiwaingiza wazee, na kusema, "Vipi?" Mnarudi kufia katika nchi ya uenyeji wenu?"

59 Kasema, "La, tumekuja kumwona Masihi."

60 Na, ndugu, nawaambia, tuko mlangano! Ndio hao watumishi, ambao wanaongojea kule ng'ambo. Si kundi hili la Wayahudi ambao wangaliwanyang'anya hata meno bandia kama

wangeliweza, hao sio Wayahudi Yeye anaonena habari zao. Bali ni wale kule ng'ambo waliotii zile—zile torati na kadhalika, na hawakujua kamwe kulikuwako Masihi.

61 Na ndugu. . .kule Stockholm, Ndugu Petrus, aliwatumia Agano Jipya milioni moja, nao walipozipata walikuwa wakizisoma. Wao walisema, "Vema, kama Huyu ndiye Masihi, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, nasi tutamwamini."

62 Ni jambo zuri vipi kwa huduma yangu! Nilikuwa umbali upatao masaa mawili kufikia malango ya Yerusalemu, kuingia, na nilikuwa kule Cairo, Misri. Nami nilikuwa nikitembea kule, na Roho Mtakatifu akasema, "Usiende sasa."

63 Nilidhani, "Nilikuwa tu nikiwaza. Nimenunua tikiti yangu nami niko njiani. Mtu yule yuko kunilaki, kundi lote, mashule na kadhalika."

64 Nikatembea mbali kidogo, na Roho akasema, "Usiende! Usiende!"

65 Nilirudi tena kwa yule muuza tikiti, nikasema, "sitaki tena tikiti hii. Nataka kwenda Athene, Uyunani, Mlima wa Mars.

66 Naye akasema, "Vema, tikiti yako imeandikwa Yerusalemu, bwana."

67 Nikasema, "Nataka kwenda Athene badala ya kwenda Yerusalemu." Roho Mtakatifu yu angoja, saa hiyo haijaja bado. Si wakati unaofaa.

68 Tazama:.

> *. . .kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.*
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi. . .hata. . .kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.* (kila mtu ajua kuwa huo ni Muhuri wa Roho Mtakatifu; tazama)
>
> *Nikasikia hesabu yao* hao *waliotiwa muhuri:. . .*(sasa, kama hao si Wayahudi, tazama hili)*. . .katika kila kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu.* (hakuna Mtaifa hata mmoja kati yao. Hapo ni mnamo wakati wa mwisho).

69 Tazama! kabila ya Yuda kumi na mbili elfu; kabila ya Reubeni, kumi na mbili elfu; na kuendelea, Gadi, kumi na mbili elfu; Naftali, na—na—na kuendelea hata kwa Asheri, na—na—Zabuloni, na haya yote makabila kumi na mawili ya Israeli. Na Kumi na mbili mara kumi na mbili ni ngapi? Mia na arobaini na nne elfu. Hao ndio wale mia na arobaini na nne elfu, Wayahudi! Si Mataifa, ni Wayahudi! Haihusu kwa vyo vyote vile Bibi-arusi. Kwa hivyo Mashahidi wa Yehova wamekosea katika fundisho lao. Biblia yasema, dhahiri kuwa hao ni "Wayahudi," si Mataifa.

Wao ni watumishi, na Mataifa hawakufikiriwa kamwe kuwa watumishi. Sisi tu wana wa kiume na wa kike, si watumishi.

70 Sasa soma yaliyobakia. Kama mtu aliyekula tikiti, alisema, "Hiyo ni nzuri, lakini tupe nyingine zaidi." Vema, Mungu anayo nyingi zaidi hapa. Naam, hebu tazama. Basi, basi tuko kwenye aya ya 8:

> *Na kabila ya Zabuloni . . . walitiwa muhuri kumi na mbili elfu. Makabila yote ya Yusufu walitiwa muhuri kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Benjamini walitiwa muhuri kumi na mbili elfu.*

71 Ona, Yohana, akiwa Myahudi, alitambua kila moja yao, aliona yale makabila kumi na mawili ya Israeli; elfu kumi na mbili toka kwa kila kabila, kumi na mbili mara kumi na mbili ni mia na arobaini na nne elfu. Ndio hao, si Kanisa, ni Wayahudi. Biblia ilisema hapa hao wote walikuwa "wana wa Waisraeli," kila kabila limetajwa.

72 Sasa tazama, aya ya 9:

> *Baada ya hayo* (sasa hapa yuaja Bibi-arusi)
>
> *Baada ya hayo nikaona, na tazama . . . mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, . . .*

73 Hao ndio matowashi wako wa hekaluni, mia na arobaini na nne elfu pekee, kundi dogo mno, walinzi wachache tu wa hekalu watakaokuwa pamoja na Bibi-arusi; ni—ni wanaomsindikiza tu. Hao ndio wale mia na arobaini na nne elfu, ndio wanaomsindikiza Bibi-arusi, matowashi wa hekalu.

74 Tazama! Bila shaka, najua unarejea hapa kwenye aya ya 14 na kusema, "Naam, hao wako na Bibi-arusi po pote wao . . . " Bila shaka! Matowashi hutembea na malkia po pote aendepo. Hakika! Bali hao walikuwa akina nani? Hawakuwa kingine ila wasindikizaji, ndivyo Maandiko hapa yasemavyo hasa.

75 Tazama:

> *Baada ya hayo . . . na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa . . . na kabila na jamaa na lugha . . .* (hao ndio yule Bibi-arusi wako wa Mataifa akija, vema) . . . *wamesimama . . . mbele za Mwana- Kondoo,* (hapo yupo Mwokozi wao, yule Mwana- Kondoo, si ile torati; yule Mwana- Kondoo, Neema) . . . *wamevikwa mavazi meupe, . . .* (tazama, katika dakika chache, oneni iwapo mavazi meupe si ile haki ya watakatifu) . . . *wana matawi ya mitende mikono mwao:*
>
> *Wakilia kwa sauti kuu . . .* (kama huu si mwamsho wa pentekoste, sijawahi kusikia hata mmoja) . . . *wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi na Mwana- Kondoo.*

Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za hao wazee na za wale wenye uhai wanne...nao wakaanguka. mbele ya kile kiti cha enzi wakamsujudu Mungu,

Wakisema, Amina, Baraka...na utukufu... nahekima...na shukrani...na heshima...na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.

76 Hayo yanaonekana kama wakati wa mkutano wa kambi, sivyo? Itakuwa hivyo! Nani hao? Wale mia na arobaini na nne elfu? Sivyo kwa vyo vyote vile! Huu mkutano mkubwa ambao hapana mtu awe...wa kila kabila lugha, na taifa. Huoni rafiki yangu mpendwa?

77 Sasa tazama hebu isome, sasa:

Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! watu hawa waliovikwa mavazi meupe...ni akina nani? Nao wametoka wapi?

78 Yule mzee akamwambia Yohana, Myahudi aliyewatambua wale mia na arobaini na nne elfu, akisema, "Naam, uliwajua, hao wote ni Wayahudi. Bali hawa ni akina nani? Nao wametoka wapi?" Mwaona alivosema yule mzee? "Akajibu mmoja wa wale wazee" (hiyo ni wale wazee walio mbele ya kile Kiti cha Enzi) "akanijibu akisema, 'Je, watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Nao wametoka wapi? Sasa, sote twawajua Wayahudi na agano lao na mengineyo, lakini hawa wametoka wapi?'" Sasa tazama:

Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. ("si—si—sijui," Yohana alisema, "yamenipita. Sijui.") *Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, iliyo kuu,* ("Kupitia kwa majaribu na hatari hizi nyingi, masumbuko na mitego nimekwisha kuja." Ona?) *wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao*...(katika kanisa? Hilo ni sahihi?)... *wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya damu ya Mwana-kondoo.*

...*wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku*...(nani anitumikiaye nyumbani kwangu? Mke wangu. Sivyo?)...*na katika hekalu lake*...(huyo ndiye yule aishiye nami nyumbani mwangu na katika kanuni zangu za nyumbani, ni mke wangu. Yeye ndiye aketiye nami, na kufua nguo zangu, na kunitayarishia mimi vitu)...*na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatandaa hema yake juu yao.*(Ee, lo, sikiza!)

Hawataona njaa tena,...(ilionekana kama kwamba walikosa milo michache safarini.)...*wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.*

> *Kwa maana huyo Mwana-kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta . . . machozi yote katika macho yao.* (ndiye huyo, ndiyo, ndiye huyo Bibi-arusi wako)

79 Ndio hawa wale mia na arobaini na nne elfu wako, ndio hao watumishi wako. Kwa hivyo "wana wa Ufalme," hapa, mtu mpendwa uliyeuliza swali hili . . . aliyeuliza swali hili muhimu. Nadhani huenda nililiacha nyuma huku katika . . . mahali fulani, lakini "watakapotupwa nje," haimaanishi kuwa watatupwa nje ya mawazo ya Mungu. Wao wanatupwa nje ya manufaa ya kiroho kwa muda fulani. Ona, kwa kitambo kidogo tu.

80 Kwa sababu, nabii alipoona ambapo Israeli angekuwa siku hizi, yeye alisema, "Vema, Israeli itakuwako Sabato itakapoondolewa, na—nao wauze katika Sabato kama tu siku zinginezo, na mambo haya yote." Yeye alisema, "Vema, uta—uta . . . Je, Israeli itasahauliwa kabisa?"

81 Yeye alisema, "Je mbingu zina urefu gani? Dunia ina kina gani? Ipime na kijiti kilicho mbele yako."

Yeye akasema, "Siwezi!"

82 Akasema, "Wala nami sitasahau Israeli kamwe." Hakika sivyo! Israeli haitasahaulika kamwe.

83 Kwa hivyo, mwaona, *daima na dawamu* ni mambo mawili tofauti, Israeli ilitupwa nje, lakini si nje ya fikara za Mungu. Na Paulo anainena hapa, kama ningekuwa na . . . ningelikuwa na wakati wa kusoma kirefu, ili nipate Maandiko upesi ambayo . . . ningewarejezeni, ona, yale yajayo mawazoni mwangu.

84 Paulo akinena pale, alisema kuwa sisi Mataifa tuangalie, jinsi tunavyoenenda na kile tunachotenda. Ona? Kwa kuwa kama Mungu hakuliachia tawi la asili, ona, tukiwa tu pandikizo, ona, . . . Na Israeli, waliopofushwa kwa muda, yeye alisema. Kwa muda tu, Israeli walipofushwa. Naam, lakini utaji ule utainuliwa toka machoni mwao. Na hapo ni wakati yule Mtaifa wa mwisho atakapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, ndipo utaji utainuliwa toka kwa macho ya Israeli. Nao watasema, "Huyu ndiye Masihi tuliyetarajia kumwona." Naam, lakini mlango wa Mataifa umekwisha kufungwa (ile safina—ime—imefungwa), hakuna tena neema iliyobaki kwa ajili ya Mataifa wakati huo.

85 Naam, nachukua muda mwingi sana kwa swali moja. Na mtu fulani asema, "Sasa hufikii langu." Vema, tutaharakisha na tuone kama tunaweza kulifikia.

86 Vema, hapa kuna mo—moja refu. Na kila fungu dogo alilouliza mwanamke au mwanamume huyu, au ye yote yule, ni sahihi.

53. Je, si ni kweli kuwa Bwana Yesu hakufia ulimwengu wote, yaani kila mtu duniani, ball . . . (sasa, ningeeleza

hilo, lakini yeye...mwanamume au mwanamke, ye yote yule...Unaonekana kama mwandiko wa mwanamke)... **bali kwa ajili ya hawa—bali kwa ajili ya hawa waliomo kote ulimwenguni, wale aliompa Baba? Hawa ambao kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu, Mungu aliwachagulia Uzima wa Milele, akisha kuwateua kulingana na mapenzi yake mema?**

87 Bila shaka hilo ni sahihi! Hilo ni sahihi hasa. Yesu aliwafia...si tu ku...Yeye amewakusudia.

88 Hebu tuone, naamini ya...na—naamini wao walisoma... swali laja kuhusu haya:

54. Maandiko bila shaka yatwambia kuwa hawa ni wale ambao hawata...ni wale ambao hawataokolewa. Kwa hivyo...

89 Hilo ni sahihi hasa. Maandiko yatwambia kuwa kunao watu waliochaguliwa awali na Mungu wapate kuhukumiwa.

90 Je, mngependa kusoma hayo, ili yawe mawazoni mwenu daima? Vema, hebu na tufungue sasa Kitabu cha—cha Yuda, Yuda akinena hapa.

> *Yuda mtumwa wa Yesu Kristo, ndugu yake Yakobo, kwa hao walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo.*

91 Mnaona Yeye alikiandikia nani? Si mwenye dhambi, si wanaofanya kazi ya uinjilisti pekee, bali waliotakaswa na kuitwa. Ona, wale walio tayari Ufalmeni.

> *Mwongezewe rehema na amani na upendano.*
>
> *Wapenzi,...nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari za wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*
>
> *Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii,*...(vipi!)... *wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi*...

92 Walioandikiwa tangu zamani! Si kwamba Mungu aliketi katika kile kiti cha enzi, na kusema, "Nitamwokoa mtu *huyu*, nitampoteza mtu *huyo*." Haikuwa hivyo! Mungu alikufa, na Yesu alipokufa ule utakaso ulifunika dunia nzima kwa ajili ya kila mtu. Lakini Mungu kwa kujua tangu zamani...Si kwamba Yeye ata...Yeye hapendi mtu ye yote apotee. Yeye alitaka kila mtu aokolewe. Hilo lilikuwa kusudi lako—hilo lilikuwa kusudi Lake la Milele. Lakini kama Yeye alikuwa Mungu, Yeye alijua nani angeokoka na nani hangeokoka. Kama Yeye hakujua, basi Yeye hangekuwa Mungu asiye na mwisho. Kwa hivyo Biblia yafundisha hayo. Kuwa tunge...

93 Kama tungekuwa na wakati wa kufungua humu katika Warumi, sura ya 8, nawe ungeisoma. Warumi, sura ya 9, mahali pengine pengi katika Biblia. Waefeso, sura ya 1. Nanyi mwaweza kuona kuwa ule uchaguzi wa Mungu, kusudi usimame imara, Mungu alitoa agano bila masharti. Yeye alimtuma Yesu afe kwa ajili ya wale wote aliotangulia kuwajua. Ona?

94 Sio kusema tu, "Vema, wasema Mungu hajui kama yeye ataokoka au la?" Mungu alijua kuwa ungeokoka, au ungeokoka au la, ulimwengu usijaanza, ama Yeye hakuwa Mungu.

95 Je, wajua maana ya neno *bila mwisho?* Tazama. . . litazame kwenye kamusi na upate maana ya neno *bila mwisho*. Naam, Yeye alijua kila kiroboto ambaye angewahi kuwa duniani, kila inzi, kila mbu, kila chembechembe hai. Yeye alijua kabla hivyo havijakuwepo, au Yeye hakuwa Mungu. Bila shaka, Yeye alijua. Naam.

96 Kisha ndani mle, Mungu hange—hangesema, "Nitakuchukua *wewe,* nikutupe kuzimuni; na nitakuchukua *wewe* nikuingize Mbinguni." Mungu alitaka ninyi mwende Mbinguni. Lakini kwa kujua mbeleni Yeye alijua kuwa mmoja angekuwa mdanganyifu, na mwingine angekuwa muungwana na Mkristo. Ona? Kwa hivyo ilimpasa kumtuma Yesu afe, kuokoa mtu ambaye Yeye alimjua mbeleni kwamba walitaka kuokolewa. Mwalifahamu?

Sasa tazama hapa:

Maandiko yanatuambia wazi wazi ya kwamba hawa ndio wale ambao hawataokoka.

55. Kwa hivyo kama ule upatanisho uliwatosha wazao wote. . . wazao wote wa Adamu, na wengine wao walipotea kwa sababu hawakujifaidishia ahadi ile, au yale maafikiano, hawange. . . lazima sisi. . . yeye ata. . . itakuwa nguvu kuu zaidi kuliko ile mipango na kusudi la Milele la Mwenyezi Mungu? Ingekuwa. . . (mtu huyu sasa kwa hili swali la pili, lasema. . .) **je, mwanadamu** (kwa hiari yake mwenyewe) **hangekuwa na nguvu kuu zaidi kuliko mipango ya milele na kusudi la Milele la Mwenyezi Mungu?**

97 La, ndugu yangu au dada. Sivyo, bila shaka! Hakuna cho chote chenye nguvu zaidi. . . Hiari ya mwanadamu haiwezi kamwe kulinganishwa na kusudi la Milele la hukumu ya Mungu. Haingewezekana, ona.

98 Sasa, swali lako la kwanza lilikuwa sahihi. Swali lako la pili halingeweza kuwa sahihi, rafiki. Kwa sababu tazama, tazama jinsi imeandikwa hapa, ona: "Hiari ya mwanadamu ingekuwa yenye nguvu zaidi ya mipango na kusudi la milele la Mwenyezi Mungu?" Naam, hakika sivyo. Hiari ya mwanadamu ingewezaje kuwa yenye nguvu kuu zaidi kuliko kusudi la Mwenyezi Mungu? Na Mwanadamu katika hali yake ya kimwili kukusudia kuchagua atakalo, kuwa na nguvu zaidi ya kile Mungu wa Milele aliye mkamilifu awezacho kuwa? Hakika

sivyo! Haingewezekana, ona. Mungu wa Milele, ambaye kusudi Lake ni kamilifu, ungesemaje kuwa mwa—mwanadamu wa kimwili hapa, haidhuru yu wa haki vipi (na huenda akawa) kusudi lake haliwezi kamwe kulinganishwa na hili, ku—kusudi la Mungu wa Milele na Mungu Mwenyezi.

99 [Dada anena toka mkutanoni—Mh.] Naam. (Nasikitika. Nilitaka tu kuuliza swali na—na ulielewa vibaya kile nilimaanisha pale.") Naam, vema, dada. (Siamini hili kamwe, nilimaanisha "kusudi la Mungu la Milele linashinda hiari ya mwanadamu.")

100 Naam. Ee, vema, ni—melisoma vibaya basi, ona. Vema. Naam, u sahihi kabisa, dada. Sikujua lilikuwa swali la—lako. Vema. Lakini, ona, ambapo nililipata hapa, ona . . . Sasa hebu nione, **"Kuwatosha uzao wote wa Adamu na wengine wao walipotea kwa sababu hawakujifaidishia wenyewe—wenyewe maafikiano yake, si hiari ya mwanadamu ingekuwa nguvu kuu zaidi kuliko mipango na kusudi la Milele la Mwenyezi Mungu?"** Ona ni—nilikuwa nimefafanua vibaya waza lako pale. Naam, lile kusudi la Milele la Mwenyezi Mungu. Vema, hiyo imetosha.

101 Nadhani kila mtu afahamu hilo. Kama ndivyo, inueni mikono yenu. Ni—kusudi la Milele la Mwenyezi Mungu, lingekuwa bila shaka juu zaidi—juu zaidi ya yale mwanadamu angetenda.

Naam;

56. Sifahamu nuru ya ubatizo wa maji, katika sura ya 28 ya . . . aya ya 19, ya Mathayo. Maana yake ni nini?

102 Vema, sasa, labda haitanichukua muda ila dakika moja hivi tu. Na hebu mtu fulani afungue pamoja nami mkiweza, Mathayo, sura ya 28, na aya ya 19. Nasi tutaona, yale tu mtu yule ana . . . ishirini na tano . . . Naam, Hili litakufanya imara kama utakaa Nalo tu. Ni—ni zuri, mwaona. Si kiingilisti, lakini ni . . .

103 Sasa tuna . . . Sasa hapa ndipo watu hujaribu kusema, "Kuna kupingana katika Biblia." Sasa, nataka mtu fulani afungue . . . pamoja na Mathayo 28:19. Au la, nataka mtu fulani . . . Mathayo 28:19. Nataka mtu fulani afungue Matendo 2:38. Je, una Biblia yako pale, Ndugu Neville?

104 Nami nawatakeni ninyi mjisomee wenyewe sasa. "Nami nitawonyesha upinzani mkali katika Biblia. Nami—ni—nataka—Biblia . . . watu husema 'Biblia haijipingi,' nataka muwazie hili."

105 Na hili lawafanya walimu wakuu wa vyuo kupata mvi. Bali ni—ni rahisi. Sasa nitasoma Mathayo 28:19, mnifuate. Na wengine wenu wenye Matendo 2:38, iwekeni tayari. Nitaanzia kifungu cha 18, hii ni sura ya mwisho ya Mathayo:

> *Yesu akaja kwao, akasema na wanafu . . . akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.* (je, mamlaka ya Baba yako wapi?)

106 Kama mamlaka yote Mbinguni na duniani yametolewa kwa Yesu, Mungu alipotewa na mamlaka basi, sivyo? Au, je, alindanganya? Yeye alikuwa akifanya mzaha? Yeye alilikusudia! Je, waamini Yeye alilikusudia? Vema, kama mamlaka yote yametolewa Kwake, je, mamlaka ya Mungu yako wapi basi? Yeye alikuwa Mungu! Ndivyo hasa. Naam, hivyo tu. Hamna lingine. Ona, Yeye alikuwa Mungu; au kama kuna mtu fulani anayeketi pale, aliyekuwa na mamlaka, hayuko nayo tena. Ona? Hivyo basi huwezi—huwezi kuitatanisha. Tutaipata hiyo humo kwa jambo lili hili. Vema:

> *. . .Mamlaka yote mbinguni na duniani nime. . . mbinguni na duniani,*
>
> *Basi, enendeni, mkawafanye. . .mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu:*
>
> *Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. . .na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*

107 Matendo 2:38, sasa mtu fulani asome. Ngoja kidogo tu. Matendo, mlango wa pili, aya ya 38. Naam, sikiza kwa makini sasa, iweni tu watulivu, nasi tutaona sasa. Naam, hizi ni siku kumi baada ya Yesu kuwambia basi, Mathayo 28:19, "Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

108 Sasa, Petro, siku kumi baadaye. . .Hawakuhubiri mahubiri mengine kamwe. Walienda kwenye chumba cha juu kule Yerusalem, na kungoja kule (kwa siku kumi) Roho Mtakatifu ashuke. Wangapi wajua hayo? Mahali hapa. Yupo hapa Petro, Petro anazo zile funguo za Ufalme, vema, tutaona atakachofanya. Mathayo. . .au namaanisha Matendo 2, hebu tuchukue kifungu cha 36:

> *Basi nyumba yote ya Israeli wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyem. . .sulubisha, kuwa Bwana na Kristo. ("Bwana na Kristo,"* si shaka alipewa mamlaka yote mbinguni na duniani)
>
> *Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na. . .mitume wengine, Tutandeje, ndugu zetu?*
>
> *Petro akawaambia,. Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

109 "Sasa, hapa kuna upinzani. Mathayo ilisema, "batizeni kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu," na Petro katika Matendo 2:38, siku kumi baadaye, "Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo."

110 Ndipo wakati unaofuata toba iliponenwa—ilipotajwa... au ubatizo, katika Biblia, ni Matendo su—sura ya 8, wakati Filipo aliposhuka kwenda na kuhubiri kwa...kwa...kwa wale Wasamaria. Nao walipokea Roho Mtakatifu, na wakabatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

111 Kutajwa kwakwe mara ya pili, ilikuwa wakati wale Mataifa walipoupokea, Matendo 10:49:

> *Petro alipokuwa. akisema maneno hayo,* tazama, *Roho Mtakatifu akawashukia... wote...* na waliwasikia.
>
> *Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu,*
>
> *Ni nani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe... watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?*
>
> *Akaamuru wabatizwe kwa jina lake BWANA* Yesu Kristo.

112 Sasa hebu nipate kitu fulani hapa niwaonyesheni jambo fulani dogo ili msiisahau; nitawaonyesha mfano mdogo. Nitaweka...Ni vizazi vingapi...Mataifa mangapi yaliyoko ulimwenguni? Kunayo matatu; watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Wangapi wajua hayo? Tunatoka kwa hao wana watatu wa Nuhu. Watu wa Hamu, watu wa Shemu...watu wa Yafethi ni Wa-Anglo-Saxon, watu wa Shemu ni...Vizazi vitatu, hivyo ni; Wayahudi, Mataifa, na walio nusu Wayahudi na nusu Mataifa. Sasa, chunguza, wakati hao...na *huyu* ni Hamu,...Shemu, Hamu na Yafethi.

113 Sasa, mara ya kwanza ubatizo uliponenwa, ulinenwa na Yohana Mbatizaji. Wangapi wajua kuwa hilo ni kweli? Vema, nitaiweka hapa, upande huu, Yohana Mbatizaji. Na Yohana aliwabatiza watu katika mto wa Yordani, akiwaamuru kuwa wanapaswa kutubu na kuwa sahihi kwa Mungu na wauze mali zao, na kulisha maskini, na wanajeshi watosheke na pesa zao, wakawe sahihi kwa Mungu. Wangapi wajua hilo? Na yeye aliwabatiza katika mto wa Yordani, si kwa kuwanyunyizia maji si kwa kuwamwagilia, bali kwa maji mengi! Kama huiamini, hapa kuna kamusi, chunguza kama si *baptizo*, ambalo ni "kubatiza, kuzamisha, tia majini kabisa, kuzika." Sasa, mara ya kwanza ubatizo uliponenwa, ilikuwa ni pale.

114 Kutajwa kwa pili kwa ubatizo, kulikuwa Yesu alipowaamuru, Mathayo 28:19.

115 Kutajwa kwingine kwa ubatizo kulikuwa ni Matendo 2:38.

116 Kutajwa kwingine ubatizo ulipotajwa kulikuwa ni katika sura ya 8 ya Matendo.

117 Kutajwa tena kwa ubatizo kulikuwa katika—katika sura ya 10 ya Matendo.

118 Na ndipo twaja kutoka wakati ule Yesu alisema, hapa, "Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

119 Sasa hebu na tunyoshe andiko lile, kwanza. Nimewaambia kuwa "hakuna hata Andiko moja katika Biblia ambalo linahitilafiana na lingine." Nawatakeni mniletee. Nimeuliza hilo kwa miaka ishirini na sita, nami bado sijalipata. Hakuna Andiko linalohi . . . Kama yanahitilafiana, basi ni ya mwanadamu-maandishi tu. La bwana, hakuna kupingana katika Biblia!

120 Sasa mwasema haya, "Na *hilo* je?"

121 Hapa Yesu yuasimama akisema, "Enedeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

122 Na Petro ageuka moja kwa moja, na kusema, "Tubuni, kila mmoja, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo."

123 "Ndio huo ukinzani wenu." Waonekana hivyo. Sasa, kama unasoma na nia ya kimwili, si na moyo mkunjufu, itakuwa ni kuhitilafiana.

124 Lakini kama utaisoma kwa moyo mkunjufu, "Roho Mtakatifu ameyaficha haya wenye hekima na akili," Yesu alisema hivyo, na Mungu ashukuriwe kwa hayo, "na amewafunulia watoto wachanga wanaotaka kujua." Kama una wazo, na si wazo la kujinufaisha, lakini moyo unaopenda kujua, Roho Mtakatifu atakufundisha mambo haya.

125 Sasa kama hailingani . . . Ulisema, "Unajuaje u sahihi?" Vema, inalingana na Maandiko mengine yote, kama hufanyi hivyo, unapata hitilafu dhahiri hapa.

126 Sasa nataka kuwaulizeni swali. Hii ndiyo sura ya mwisho Mathayo. Nitachukua kwa mfano mdogo, ili kila mmoja wenu . . . watoto wataelewa.

127 Kwa mfano, ukisoma hadithi ya mapenzi, na mwisho wake ilisema, "Nao Mariamu na Yohana wakaishi kwa raha mustarehe." Vema utashangaa huyu Yohana na Mariamu walioishi kwa raha mustarehe ni kina nani. Basi, iwapo unataka kujua Yohana na Mariamu ni nani, utarudi nyuma mwanzoni mwa kitabu na kuona hawa Yohana na Mariamu ni nani. Ndipo rudi hapa nyuma ukaone Mariamu alikuwa nani, naye anatoka kwa jamaa gani, na Yohana alikuwa nani, naye anatoka kwa jamaa gani, na jina lake lilikuwa nani, na walivyooana, na mengineyo yanayowahusu. Sivyo?

128 Vema, vivyo hivyo katika kusoma Biblia hapa. Wakati . . . Tazama, Yesu hakusema kamwe, "Enendeni mkawabatize watu katika jina la Baba, katika jina la Mwana, katika jina la Roho Mtakatifu," jinsi watu wa utatu wabatizavyo. Hakuna Andiko kama hilo katika Biblia. Yeye hakusema kamwe, "Katika majina (m-a-j-i-n-a) majina" ya Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.

129 Yeye alisema, "Kwa (j-i-n-a) jina," umoja. Tazameni katika Biblia zenu hapo na mwone kama sivyo, Mathayo 28, "Kwa *Jina*."

130 Si "Kwa jina la Baba, kwa jina la Mwana . . . " hivyo ndivyo wahubiri wa utatu wabatizavyo. "Kwa jina la Baba, kwa jina Mwana, na kwa jina la Roho Mtakatifu." Hiyo hata haimo katika Biblia.

131 "Ndipo kwa jina . . . " Ulisema, "Vema, basi kwa jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Basi kuna jina fulani hapo.

132 Naam, je, Baba ni jina? Wangapi wajua Baba si jina. Baba ni sifa. Mwana si jina. Wangapi wajua kuwa mwana si jina? Baba wangapi walio humu? Inueni mikono yenu. Wana wangapi waliomo humu? Inueni mikono yenu. Vema, wangapi wenu mmepewa jina "mwana?" Wangapi wenu mmepewa jina "baba?" Vema. Roho Mtakatifu si jina. Roho Mtakatifu ni jinsi alivyo. Wanadamu wangapi walio ndani humu? Inueni mikono yenu. Ona Naam, Roho Mtakatifu ni jinsi alivyo Baba, mwana, na Roho Mtakatifu, hayo si majina; hamna majina kwao.

133 Vema, basi, kama Yeye alisema, "Batizeni kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu," yatupasa kurundi nyuma kuona Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nani. Hebu tufungue sura ya kwanza ya Mathayo basi, tuone mtu huyu alikuwa nani na tunapaswa kubatiza kwa jina gani. Nasi tutaanzia sasa na Mathayo, sura ya kwanza, na aya ya 18. Someni kwa makini ninyi nyote.

134 Basi, wewe uliyeuliza swali hili, nataka kutoa mfano mdogo hapa. Naam, nitaweka vitu vitatu hapa ili ufahamu dhahiri, (kutoa mfano) Biblia hizi na vitabu hivi, kutoa mfano.

135 Vema, nawatakeni mniangalie kwa makini, na kila mmoja anifuate sasa. Sasa, *Hiki* hapa ni Mungu Baba. *Hiki* hapa ni Mungu Mwana. *Hiki* hapa ni Mungu Roho Mtakatifu. Sasa, wangapi wanaelewa? Semeni nyuma yangu. Huyu ni nani hapa? [kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu,"—Mh.] Roho Mtakatifu. Huyu ni nani hapa? [kusanyiko linasema, "Baba"—Mh.] Huyu ni nani hapa? [kusanyiko linasema "Mwana"—Mh.] Sasa, hivyo ndivyo watu waaminio utatu huamini. Ona, hilo latufanya makafiri, makafiri watupu.

136 Wayahudi; hiyo ndiyo sababu huwezi kumwambia Myahudi lo lote. Yeye alisema, "Huwezi kumkatakata Mungu katika vipande vitatu na kumpa Myahudi." Lakini, sivyo hakika, hata nami huwezi. Ona? La, bwana. Yeye ni Mungu mmoja. Ndivyo hasa. Si miungu mitatu. Sasa tazama jinsi—jinsi ilivyo rahisi.

137 Sasa tutachunguza, sasa, nani . . . *Huyu* ni nani? Wengine waseme sasa. Mungu Mwana. Sivyo? *Huyu* ni Mwana. Vema, basi baba Yake ni Mungu. Sivyo? Wangapi wanaamini kuwa baba Yake ni Mungu, inueni mikono yenu. Wangapi wanamini kuwa Mungu ni Baba wa Yesu Kristo? Vema.

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi . . .

138 Sasa tunarudi nyuma kuona Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nani, ambao Mathayo alisema "mkabatize kwa Jina la." Ona, Jina; si majina sasa, kwa sababu haiwezekani kuwa ni majina, kwa kuwa hamna jina pale.

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu . . . mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa* Mungu Baba. (Je, Biblia inasema hivyo? Biblia yasemaje?) . . . *alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*

139 Basi nani kati ya *hawa* aliye Baba Yake? Sasa, Biblia ilisema kuwa *huyu* ndiye baba Yake, na Yesu alisema kuwa huyu ndiye baba Yake. Basi, Baba Yake ni yupi? Naam, kama yeye alikuwa na baba wawili, vipi basi? Kama Yeye alikuwa na Baba wawili, Yeye ni mwana haramu.

140 Hebu tuendelee kusoma tena:

> *Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.*
>
> *Bali alipokuwa akififikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa* . . . [kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu"—Mh.]

141 Nani? Roho Mtakatifu? Vema, Baba awezaje kuwa ndiye baba Yake, na Roho Mtakatifu awe baba vile vile? Sasa, Yeye alikuwa na baba wawili basi, kama hilo ni kweli. La, bwana! Roho Mtakatifu ni Mungu. Roho Mtakatifu ni Mungu. Kwa hivyo Mungu na Roho Mtakatifu ni Mtu yule yule, ama Yeye alikuwa na baba wawili.

142 Tuone kama twaweza kutambua *Yohana na Mariamu* ni nani, baada ya muda mfupi. Vema, tuone kama Petro na Mathayo walikuwa wakijaribu kuhitilafiana wao kwa wao au la, tuone kama Maandiko yanahitilafiana. Ni ukosefu wa ufahamu wa kiroho. Naam.

Basi alipokuwa akifikiri hayo . . .

143 Nilisoma hayo, aya ya 20. Sasa ya 21:

> *Naye atazaa mwana* . . . (mtu huyu aliyekuwa wa Nafsi Moja, Mungu) . . . *nawe utamwita jina lake* . . . (nani?) [kusanyiko linajibu "Yesu"—Mh.] . . . *maana yake, ndiye atakayeokoa watu wake na dhambi zao.*
>
> . . . *hayo yote yamekuwa, ili* . . . *litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema,*

> *Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani Mungu pamoja nasi.*

144 Kwa hivyo *Yohana na Mariamu* ambao waliishi kwa raha mustarehe walikuwa kina nani? Ni nani aliyesema, "Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu?" Baba alikuwa nani? Lile Jina Baba na Mwana na Roho Mtakatifu? [Mtu fulani asema, "Yesu"—Mh]. Bila shaka. Hakika, hamna hitilafu hapo. Hata kidogo. Hilo ladhihirisha Maandiko. Yeye alikuwa ndiye Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu. Mungu alikuwa (Imanueli) akikaa pamoja nasi, akiishi katika mwili ulioitwa "Yesu."

145 Sasa yale mafundisho ya umoja ya kanisa la Oneness, hakika sikubaliani nayo, kuwaza ya kwamba Yesu ni mmoja kama kidole chako kilivyo kimoja. Ilimpasa Yeye awe na baba. Kama sivyo, Yeye angekuwaje baba Yake mwenyewe? Na kama Baba Yake alikuwa mtu kama wa utatu wasemavyo, basi yeye alizaliwa haramu kwa baba wawili. Hivyo basi, mwaona, ninyi mmekosea kwa kubishana. Ona?

146 Lakini Kweli yake ni kwamba, wote Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu ni Nafsi moja. (Nafasi tupu kwenye ukanda Mh.] . . . ya kuishi katika maskani ya mwili, kuondoa dhambi ulimwenguni. Naam hasa, "Mungu pamoja nasi." Sasa, hivyo basi, wakati Mathayo 28:19 . . .

147 Naam, chunguzeni Maandiko, mkipata ambapo mtu mmoja katika Biblia . . . (sasa, liwaze, sasa usiruhusu hili likupite) . . . ambapo mtu mmoja katika Biblia alibatizwa katika jina la "Baba," na la "Mwana," na la "Roho Mtakatifu," rudini kwangu mkaniambie kuwa mimi ni mnafiki, nami nitaweka ubao mgongoni na nizunguke kote mjini. Haimo Maandikoni, tangu Mwanzo hata Ufunuo. Lakini kila mtu katika Biblia alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo!

148 Mwasema, "Ngoja kidogo, mhubiri. Na Yohana Je? Yeye hakubatiza kwa jina liwalo lote!"

149 Vema, tuone kile kilichotendeka; hebu tufungue Ma—Ma—Matendo, sura ya 19. Hapo ndipo tunawapata wanafunzi wa Yohana. Kila mtu alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo, kote hata sasa tunapoona kundi hili hapa. Matendo mlango 19. Na hebu tuanze kusoma sasa, nasi twapata wanafunzi wa Yohana:

> *Ikawa . . . ikawa Apolo* (aliyekuwa mwanasheria, aliyeongoka) *alipokuwa Korintho, Paulo akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika . . . Efeso; akakutana na wanafuzi kadha wa kadha huko;* (wao walikuwa wafuasi wa Yesu)

150 Kama ulitambua katika sura iliyotangulia hiyo, walikuwa na furaha tele hata walipiga shangwe na kufurahi. Wangapi wajua hilo ni kweli? Na Akila na Prisila walikuwa wamehudhuria

mkutano huo. Na Paulo na Sila walipigwa na kuvuliwa nguo, na kutupwa gerezani. Sivyo? Nao wakaja hapa, na kuwapata Akila na Prisila. Nao walikuwa wana mkutano wa ufufuo juu pale pamoja na mhubiri Mbaptisti, kwa jina Apolo, aliyekuwa akithibitisha kwa Maandiko kuwa "Yesu ni Kristo." Sasa Paulo ampata:

> . . .*Paulo akiisha kupitia kati ya nchi za juu, za*. . . *Efeso*. . .*akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko:*
>
> . . .*Akawauliza, Je! mlipokea Roho Mtakatifu* tangu *mlipoamini?*

151 Sasa, ninyi marafiki wapendwa Wabaptisti, kama hilo halibomoi—msingi wa theologia *yenu*, mnaposema "mlipokea Roho Mtakatifu *mlipoamini*."

152 Lakini Paulo alitaka kuwauliza hawa Wabatisti, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Sasa tazama yale waliyoyasema:

> . . .*Wakamjibu*. . .*hata hatujui kwamba kuna Roho Mtakatifu.*
>
> *Akawauliza, Basi*. . .(sasa, ukitaka kupata kamusi ya Kiyunani hapa, itakuonyesha, "Basi mlibatizwa jinsi gani?"). . .*Basi mlibatizwa*. . .*kwa ubatizo gani? Wakasema,* kwake, ubatizo wa Yohana humu. Yohana alitubatiza sisi.

153 Sasa nataka kuuliza: kama mlipokea ubatizo huo, mngetoshelezwa nao? Mtu yule yule aliyempokea Yesu mtoni, na kumbatiza Yesu Kristo, mtu yule yule alikuwa amewabatiza watu hawa. Huo ni ubatizo mzuri sana; si kunyunyiziwa maji, wala kumwagiliwa, bali kwa kutumbukizwa katika Yordani wa kale wenye matope, mahali pale pale Yesu alibatiziwa. Waza hilo.

154 Paulo alisema, "Mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Wao. . .yeye. . .

Wao walisema, "Wala. . .hatujui kama kuna Roho Mtakatifu."

Yeye alisema, "Mlibatizwaje?"

Wakasema, "Tumebatizwa."

"Mlibatizwaje?"

"Ubatizo wa Yohana!"

155 Sasa tazama kile Paulo alisema. Tazama hapa:

Ndipo *Paulo akasema*. . .mlibatiswa kwa. . .Yohana. . . Nao. . .

Paulo akasema Yohana alibatiza kwa ubatizo wa. . . ubati. . .*wa toba, akiwaambia*. . .*watu*. . .*wamwamini Yeye atakayekuja nyuma yake yaani Yesu Kristo.*

156 Ona, Yohana alibatiza tu ubatizo *wa* toba, bali ubatizo wa maji katika Jina la Yesu ni kwa ondoleo la dhambi. Utakaso ulikuwa haujafanywa wakati huo, dhambi hazingeondolewa. Sasa. . . lilikuwa tu tendo la dhamiri njema, kama chini ya torati. Luka 16:16, ilisema, "Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana; tangu wakati huo Ufalme hutangazwa." Sasa tazama, na chunguza.

Na Paulo akasema ta. . . (sasa tazama). . .*Mmepokea*

157 Aya ya 5-cha 5:

Waliposikia haya; wakabatizwa (tena) *kwa jina la Yesu Kristo.*

158 Sivyo? Basi watu hawa, watu hawa katika Matendo 2, walibatizwa kwa Jina la Yesu. Wayahudi walibatizwa kwa Jina la Yesu. Mataifa walibatizwa kwa Jina la Yesu. Na kila mtu katika Biblia nzima alibatizwa kwa Jina la Yesu.

159 Sasa, tafuta mahali pamoja ambapo mtu ye yote alibatizwa kwa njia nyingine iwayo yote, nami nitarudi papa hapa na kukuonyesha ambapo kanisa Katoliki linakubali haya, na kusema kuwa wanakubaliana nayo. Wanasema, "Huenda kukawa na baadhi ya Waprotestenti watakaookoka kwa sababu wana mafundisho machache ya Kikatoliki, kama ubatizo kwa jina la 'Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu'; ambapo kanisa takatifu Katoliki lina uweza wa kugeuza ibada hiyo toka kwa Jina la Yesu, hata kwa 'Baba, Mwana na Roho Mtakatifu,' na kanisa la Kiprotestanti lakubaliana nalo." Hili halikubaliani, nitashika ya Biblia. Naamini Biblia.

160 Wasema, "Ndugu Branham, unawaagiza watu wabatizwe tena?" Bila shaka! Paulo alifanya vivyo hivyo hapa.

161 Sasa tazama, hebu tufungue Wagalatia 1:8, tuone yale Paulo alisema:

. . .*ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo*. . . *na alaaniwe.*

162 Naam, "Ijapokuwa sisi au malaika." Na Paulo, mtu yule yule, aliwaamuru watu wabatizwe tena waliokuwa na ubatizo bora zaidi kuliko ulio nao, ndugu yangu; kwa kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa binamu wa Yesu, binamu wa karibu; akimbatiza binamu wake katika mto Yordani, na akageuka na kubatiza wanafunzi wa Yohana. Na Yesu alisema, "Huo haufai!" Samahani, Paulo ndiye alisema hayo, na kuwaagiza wabatizwe tena kwa jina la Yesu kabla hawajapokea Roho Mtakatifu; baada ya wao kupiga shangwe na kumsifu Mungu na kufurahi, wakiwa na mkutano wa ufufuo mkuu mno, na kuthibitisha kwa Biblia (kwa theologia

yao) kuwa Yesu alikuwa ndiye Kristo. Wangapi wanajua hayo ni Maandiko? Sura ya 18. Bila shaka. Naam. Kwa hivyo hamna swali kwake.

163 Sasa hebu nikupeni jambo muhimu. Sasa, yeye hakwenda nje ya utaratibu, lakini Luka. . .Mathayo, sura ya 16. Yesu, waliposhuka toka mlimani, Yeye alisema, "Watu waninena Mimi Mwana wa Adamu kuwa nani?"

164 "Wengine husema wewe u 'Eliya,' na wengine husema Wewe 'manabii,' na wengine husema wewe *'hiki, kile.'*"

165 Yeye alisema, "Nanyi mwasemaje?"

166 Petro alisema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

167 Tazama! "Heri wewe Simoni Ba-yona (mwana wa Yona), mwili na damu havikukufunulia Hili kamwe. Amina!

168 Ona, lazima ije kwa ufunuo wa kiroho. Mwili na Damu havikumwambia Habili kuwa alikuwa amekosea (Kaini, kuwa amekosea), havikumwambia Habili kuwa "Kaini alikosea." Lakini ilikuwa ule ufunuo aliokuwa nao Habili, "Ilikuwa ni damu!" tunafikia swali hilo katika dakika chache. Ilikuwa ni damu, si tunda, iliyotuondoa katika Bustani ya Edeni. "Ilikuwa ni damu," na Habili, kwa ufunuo wa kiroho. . .alifunuliwa na Mungu kuwa ilikuwa damu. Naye, kwa imani. . .Waebrania 11:1 yasema, "Alimtolea Mungu sadaka iliyo bora zaidi ya Kaini. Ndipo, Mungu akakubali sadaka yake." Naam. Ona, yeye alitoa kwa imani, kwa ufunuo.

169 Sasa tazama, "Mwili na damu havikukufunulia hili," (moja kwa moja hata kwa Bwana Yesu) "Bali Baba yangu aliye Mbinguni amekufunulia Hili. Na juu ya mwamba huu (ufunuo wa Yesu Kristo). . .Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Ufunuo wa ki-. . ."Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, nitakupa wewe funguo za Ufalme. Na lo lote. . .Kwa sababu umepata mfereji wazi wa kiroho kati ya hapa na Mbinguni. Mwili na damu: hukuyapata katika seminari, hukuyapata shuleni, hukuyapata kwa so—so—somo la theologia. Bali ulimtegemea Mungu, na Mungu akakufunulia, na inalingana na Maandiko kabisa. Nasema wewe ndiwe Petro, naam, nami nitakupa funguo; na ufungalo duniani, nitalifunga mbinguni; ufungualo, nitalifungua Mbinguni."

170 Na Petro alikuwa mnenaji kwenye Siku ya Pentekoste, wote walipokuwa wameogopa kunena, alinena na kusema. "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikize Maneno yangu. Watu hawa hawakulewa, kama mdhanivyo, kwa sababu ni saa tatu ya mchana, lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli. 'Itakuwa siku za mwisho', asema Mungu, 'nitawamwagia watu wote Roho Yangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri. Naam, nitawamwagia watumishi wangu

waume kwa wanawake Roho Yangu. Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na nchi, na nguzo za moshi na mvuke itakuwa, kabla ya kuja ile Siku ya Bwana iliyo kuu na kuogofya, kwamba ye yote atakayeliita Jina la Bwana ataokoka.'" Naam, Jamani!

171 "Muniwie radhi, niseme habari za baba yetu mkuu, Daudi," yeye akasema, "ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata hata sasa. Basi kwa kuwa nabii, yeye aliona... Yeye alimwona akiwa upande wa mkono Wake wa kuume, 'Nami sitatikika. Tena mwili wangu nao utakaa katika tumaini maana hataiacha roho Yangu katika kuzimu, wala hatamtoa Mtakatifu Wake aone uharibifu."

172 "Na Daudi amefariki," yeye alisema, "akazikwa, na kaburi lake liko kwetu leo. Basi kwa kuwa ni nabii, yeye aliona kule kuja kwa Yule Mwenye Haki, ambaye Mungu amemfanya Bwana na Kristo." Jamani! Ndiyo hayo Maandiko yenu. Hivyo ndivyo. Naam, ndivyo,

173 Sasa twaona hapa, basi, hiyo ndiyo njia sahihi, na njia halisi, na njia pekee iliyoamriwa...Na Petro alikuwa na ule ufunguo, na siku aliyohubiri, wao walisema...Sasa tazama, Kanisa la kwanza ndilo hili hapa. Ninyi Wakatoliki sikizeni Hili. Enyi wa-Campbellite sikizeni Hili. Enyi Wabaptisti na Wamethodisti sikizeni Hili. Enyi Church of God, Nazarene, Pilgrim Holiness, sikizeni Hili.

174 Petro alikuwa na ule funguo, naye alikuwa na mamlaka, au Yesu alisema uongo. Naye hawezi akasema uongo, "vitu viwili visivyoweza kubadilika," Mungu hawezi kusema uongo. Yeye alikuwa na zile funguo. Yesu alimpa funguo. Alipofufuka si-siku ya tatu hivyo, alikuwa na funguo za mauti na kizimu, lakini si funguo za Ufalme. Petro alikuwa nazo! Ndivyo hasa.

175 Na sasa tahadhari, Petro, una funguo zinazoninginia kando yako, na unahubiri. Swali laja, waongofu wa kwanza wa lile kanisa jipya. Kanisa la kwanza la kikristo. Basi enyi wakatoliki, naam, Wabatisti, wae Wamethodisti, Wapresbiteria, je mko na Fundisho la Kanisa Jipya? Chunguzeni kama ndivyo.

> ...*Tutendeje, ndugu zetu?*
>
> ...*Petro* akasimama akawaambia...*tubuni*...*kila mmoja wenu*...(wee, jihadhari, jinsi uingizavyo funguo hizo hapa, Kristo ataziingiza hivyo Mbinguni)... *Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo*...(hivyo ndivyo uingiavyo katika Hili)... *mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

176 Funguo zile ziliingia "ki" hapa, na zikaenda "ki" pale. Hivyo ndiyo sababu iliwapasa wanafunzi wa Yohana kuja wabatizwe mara ya pili, tena, kwa Jina Lake Yesu Kristo (kabla wao hawajaingia Mbinguni), wapate Roho Mtakatifu. Yeye alitimiza

Neno Lake. Kwa hivyo haiwatatanishi tena sasa, sivyo? Ona? Bila shaka, Mathayo 28:19 vilikuwa vyeo, si Jina.

177 Vema, tuna wakati gani uliobaki? Je, twaweza kupata tena dakika kumi na tano zaidi kujibu maswali mengine zaidi upesi sana? Twaweza? Vema, tutaharakisha upesi sana. Ninayo mawili hapa chini, niliyotaka kuyachukua upesi, yanafanana sana na hili kama ningeweza. Ndipo naweza kujibu yote yaliyobakia Jumapili asubuhi.

57. (a) Je, Kaini alikuwa mzao wa nyoka?(Hili ni nzuri) Kama ndivyo, je, mbona Hawa hakuchukua mimba hata baada ya Adamu kujuana naye?

Vile vile . . . swali linalofuata ni lile lile:

58. (b) Je, uli—ulikuwa mti halisi ambamo Hawa alikula lile tunda? Yeye aliona kuwa unafaa kwa chakula.

178 Vema, ndugu, dada, ye yote yule, hebu na turudi nyuma katika Mwanzo na tuone kitu fulani hapa. Hebu tufungue Mwanzo 3:8, mkiweza. Vema, na sikizeni kwa makini sasa.

179 Sasa nitaeleza hadithi hiyo. Ilikuwa safi na takatifu, hapakuweko dhambi wala unajisi. Sasa tutachukua lile . . . lako . . . hili swali la kwanza. Mti katika maisha . . . katikati ya bustani, katikati ya mti. Ule *mti* ulikuwa "mwanamke." Sasa nitathibitisha hilo kwenu kwa kutumia Maandiko mkitulia kwa dakika chache.

180 Tutaona kwanza kama yeye alikuwa . . . kama yeye alichukua mimba kabla hajajuliwa na Adamu au la, au kabla . . . sikiza:

> *Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustani wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone.*
>
> *Bwana . . . akamwita Adamu, akamwambia . . . Uko wapi?*
>
> *Akasema, Nalisikia sauti yako bustani, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi . . .* (sasa, yeye hakujua kuwa siku moja kabla, kitu fulani kilikuwa kimetendeka, kitu fulani kilichomfunulia kuwa yeye alikuwa uchi) . . . *nikajifiche.*
>
> *Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti . . . ?*

181 Je, kule kula matunda kulimfanya atambue kuwa yeye ni uchi? Kama nisemayo kila mara, (huu si mzaha, sikusudii kufanya mzaha) "Bali kama kula matofaa kuliwafanya wanawake watambue kuwa walikuwa uchi, inatupasa kuwapa matofaa tena." Ona? Haikuwa uchi . . . Haikuwa mti, tofaa, waliyokula, ilikuwa kujuana kimwili. Tazama:

> . . .*Je! umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?*
>
> *Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa*. . .*matunda ya mti huo, nikala.*
>
> *Bwana Mungu*. . .*akamwambia mwanamke, Nini hill ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya*. . .(enhee?). . .*Nyoka alinidanganya, nikala*. (Muda mrefu kabla yeye hajapata mimba, ona kwa Adamu)

182 Adamu akamjua, naye akapata mimba akazaa—akamzaa. Habili.

183 Lakini nataka kuwauliza ninyi, kwa fikira za kawaida tu. Naam, kuwathibitishia ninyi kwamba mwanamke ni mti wa matunda. Wangapi wajua hilo? Si wewe ni tunda la mamako? Bila shaka, ndivyo ulivyo. "Na katikati ya tunda, au katikati ya mti, tunda ambalo hapaswi kugusa."

184 Ukichunguza, si Yesu alikuwa ule Mti wa Uzima? Yeye aliahidi kule katika Mathayo Mt. . . . au Yohana Mt. sura ya 6, "Mimi ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni?"

185 Mwanamume akila mwanamke. . .Na tazama, kwa kuzaliwa kwa. . .na mwanamke, sote hufa; kwa sababu mauti inatutawala (sivyo?) kwa kuzaliwa na mwanamke. Kwa kuzaliwa na mwanamume, sote tutaishi milele. Mwanamke ni mti wa mauti, mwanamume ni mti wa uzima; kwa maana mwanamke hata hana uhai ndani yake. Naam hasa. Ile—ile mbegu ya uhai hutoka kwa mwanamume, sawa. Inamwendea mwanamke, na mwanamke si kitu ila chombo cha kuatimia; na mtoto hajaunganishwa, ila tu kwa kitovu. Hamna hata tone moja la damu ya mama *katika* mtoto mchanga; amezaliwa damuni mwake, bali hamna hata tone moja katika mtoto huyo. Enda kachunguze. . .au kasome vitabu vya daktari, au mwulize dakatari wako, utaona. Haimo, la, bwana, angaa tona moja la damu. Yeye ni yai tu, hivyo tu. Na uhai hutoka kwa mwanamume.

186 Huo ni mfano mzuri kuonyesha kuwa kwa mwanamke, kuzaliwa kwa kawaida, sote hatuna budi kufa, kwa kuwa ni wafu tangu mwanzo; na ni kwa Mwanadamu Kristo Yesu pekee ndipo twaweza kuishi. Na hiyo ndiyo ile miti miwili katika Bustani ya Edeni. Je humuioni?

187 Na tazama! Na katika siku hiyo kukawekwa Kerubi kulinda mti huu. Maana kama wangeuonja huo Mti wa Uzima, wangaliishi milele. Wangapi wanajua hilo? Wote wangeishi milele. Na wakati wa kwanza wangeuonja. . .Malaika alisema, "Tutaulinda." Na wakaweka Makerubi pale wenye panga za moto upande wa mashariki kuulinda. Wao waliurudisha

Mashariki, na kuulinda Mti huo kwa panga zinazong'aa wasiingie tena waupate (Mti huu).

188 Na Yesu alipokuja, Yeye alisema, "Mimi ndimi Chakula cha Uzima, na mtu alaye chakula hiki hatakufa kamwe." Huo ndio Mti wenu.

189 Huyo ndiye mwanamke wenu, huko ndiko kujuana kimwili kwenu kuletako mauti. Kwa hakika tu vile kunayo tamaa ya kujuana kimwili, kuna mauti inayosababishwa nayo. Na kwa hakika kama kulivyo na kuzaliwa kiroho kuna Uzima wa Milele unaoletwa nako. Mauti huja kwa uzazi wa mwanamke, na Uzima huja kwa uzazi wa Mwanamume. Amina. Naam.

190 Sasa hebu turudie Kaini. Je, mwaweza kuniambia ambako roho huyo na uchoyo huo ulikotoka? Kama Kaini . . . tazama, je, kama Kaini alikuwa mwana wa Adamu aliyekuwa mwana wa Mungu, uovu huo ulitoka wapi? Kitu cha kwanza yeye alipozaliwa, alichukia, alikuwa muuaji, alikuwa mwenye wivu. Na sasa chukua tabia ya baba yake, mwanzoni kabisa, Nyota ya Asubuhi, naye alikuwako tangu mwanzo . . . yeye alimwonea wivu Mikaeli, ambayo ilisababisha ile shida yote. Wangapi wajua hayo? Na Kaini alikuwa na tabia ya baba yake, ambaye alimwonea wivu ndugu yake na kumuua. Hiyo . . . tabia hiyo haingetoka kwa yule Mzao halisi. Ilitoka . . . hapana budi ilitoka kwa ukoo wake uliopotoka. Na mtazame Kaini mara tu yeye alipozaliwa.

191 Na ndipo Habili akazaliwa baada yake, ndipo akachukua mimba kwa Adamu, a Adamu akamjua—akamjua na akamzaa Habili. Na Habili alikuwa mfano wa Kristo; na Habili alipo-alipouawa, Sethi akachukua mahali pake, kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo, katika mfano.

192 Lakini sasa, Kaini aliabudu; kazi zake zote za kimwili, kama tu zile za kanisa la kimwili siku hizi; wao huenda kanisani, wanaabudu. Kaini aliabudu; yeye hakuwa kafiri, hakuwa mkomunisti. Kaini alikuwa mwamini, alimwendea Mungu, akajenga madhabahu. Yeye alifanya kila kitu cha kidini ambacho Habili alifanya, bali hakuwa na ufunuo wa kiroho wa mapenzi ya Mungu. Jina la Mungu libarikiwe! Naam. Mwaiona? Yeye hakuwa na ufunuo wa kiroho, na hiyo ndiyo shida ya Kanisa siku hizi. Na Yesu alisema Yeye angejenga Kanisa Lake juu ya ufunuo wa kiroho. Mwaifahamu? Jamani, macho yenu yaweza kufunguka sasa. Ona, ule ufunuo wa kiroho.

193 Kaini akaja akajenga madhabahu, akaabudu, akatoa sadaka akapiga magoti, akamsifu Mungu, akamwabudu Mungu, yeye akafanya kila kitu cha kidini ambacho Habili alifanya. Na Mungu akamkataa kabisa kwa sababu hakuwa na ufunuo wa kiroho!

194 Ufuate huo ukoo wa Kaini: hata kwenye safina, tangu safina hata kwa Israeli, tangu Israeli hata kwa Yesu, na tangu Yesu

hata siku hizi; na kuona kama kanisa lile la kimwili, la kiasili, vuguvugu na baridi, la kielimu, namaanisha watu walio na Maandiko, wajuao mafundisho yote na theologia na wanaweza kuieleza, wee, kama [Ndugu Branham adata kidole chake—Mh.] Hivyo, bali bila ufunuo wa kiroho! Hiyo ni kweli. Hayo ni mafundisho ya Kaini.

195 Biblia ilisema, "Ole wao! Kwa kuwa waliyaendea mafundisho ya Kaini, wakamkimbilia kosa la Balaamu, na kuangamia kwa uasi wa Kora." Kitabu kile kile, Yuda, yeye alisema, "Walichaguliwa asili kwa hukumu hii." Hakika, naam. Ona? Balaamu alikuwa nani? Alikuwa askofu. Yeye alikuwa ikisimamia kanisa lote. Akaja pale wa kiasili tu kama angeweza kuwa. Alitoa. . . Mtazame amesimama pale kwenye watu Mashuhuri, amesimama pamoja na waheshimiwa. Nao hawakuwa makafiri, walikuwa waamini.

196 Hilo—hilo kabila la Moabu lilitokana na binti wa Lutu. Lutu aliyeishi. . . Binti wa Lutu aliyeishi na babaye na akachukua mimba na kuzaa mwana na huyo mwana alikuwa. . . alianzisha kabila la Moabu. Nao walikuwa dhehebu kuu. Watu wakuu, wenye fahari, waliokuwa na watawala na wafalme na waheshimiwa. Walikuwa na maaskofu na makardinali na kadhalika.

197 Na hapa kukaja kundi la watakatifu wanaojigaragaza, lile kundi lingine, Israeli; kundi ndogo la kale ambalo halikuwa la kidhehebu, si dhehebu. Nao walifanya kila kitu kilichokuwako kwenye ramani, kibaya pia. Bali ilivyokuwa, walikuwa na ufunuo wa kiroho, na Mungu alikuwa pamoja nao katika Nguzo ya Moto.

198 Ee, ni—najua wao walikuwa na mambo ya kimwili, na watu walisema, "Kundi hoe hoe kama hilo, hakuna lingine ila kuwafukuza." Lakini wao walikuwa na ufunuo wa kiroho, hao walikuwa na Mwamba uliogongwa, walikuwa na nyoka wa shaba, walikuwa na Nguzo ya Moto iliyoandamana nao. Haleluya! Najua mwa—mwadhani nina tahamaki, bali sivyo. Najisikia tu vizuri.

199 Tazama! Niwazapo, "Mungu yule yule leo, yuaishi pamoja nasi." Ingali ni ufunuo wa kiroho wa Neno. Bila shaka. Ni sahihi Milele. Jina la Bwana libarikiwe! Naam, bwana.

200 Ndiyo huyo pale pamoja na lile kundi la kiasili, hao kundi la Wabatisti na Wapresbiteria walisimama mlimani, na kumleta askofu wao pale. Nao walikuwa tu wa kidini, na wa dini ya aina ile ile, walimwabudu Mungu yule yule. Wakasema, "Tazama chini pale hilo kundi ovyo. Naam, hata hawana dini. Wao si kitu ila kundi la wapayukaji, wapiga mayowe, watakatifu wanaojigaragaza."

201 Sivyo? Hakika, walikuwa hivyo. Usipoamini walikuwa watakatifu wanaojigaragaza, ifuatilie katika Mwanzo uone

walipovuka. Na muujiza ulifanywa, na Miriamu akashika tari akienda ukingoni akicheza tari; akicheza katika Roho na Musa akaimba katika Roho. Kama hilo si kundi la wale tuwaitao huru . . . watakatifu wanaojigaragaza, sijui ni nini basi, wakiimba na kurukaruka na kusifu. Na mataifa yaliwachukia daima, bali Mungu alikuwa pamoja nao. Wao walikuwa na ufunuo wa kiroho, waliokuwa wakifuata hiyo Nguzo ya Moto.

202 Na Moabu walisema, "Sasa, tazameni hapa. Tutawaita makardinali wote na maaskofu wote, na wazee wote, na tuwalete hapa, tutawatendea jambo fulani, sisi ni taifa la kidini. Hatutaruhusu porojo hizo zichangamane na dhehebu letu safi."

203 Na kwa hivyo ndio hao pale. Nao wakajenga madhabahu kumi na mawili; hayo ndiyo hasa yale Israeli walikuwa nayo, madhabahu kumi na mawili. Hao wakaweka dhabihu kumi na mbili juu yake, mafahali; yale hasa Israeli iliyokuwa nayo, yale Mungu alihitaji. Wakaweka kondoo kumi na wawili juu yake, wakiwakilisha kule kuja kwa Bwana Yesu Kristo; kondoo kumi na wawili katika mahali pote pawili.

204 Watu wote mashuhuri, maaskofu na kadhalika, wakazunguka pale. Waliwasha dhabihu. Wakaomba, wakamwinulia mikono Yohava na kusema, "Yehova, tusikie!" Walikuwa wakijaribu kufanyaje? Na yule mzee Balaamu alijitokeza hivyo, na Roho akamshukia. Naam (lakini yeye alikuwa wa kimwili).

205 Roho anaweza kumshukia manafiki, Biblia ilisema. Mlinisikia nikifundisha hilo, basi. "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki. Lakini lazima ilinganishwe na Neno, hapo ndipo ulipatapo.

206 Ndipo alipofanya hivyo, naye . . . Roho yule juu yake alipomwambia Kweli. Alijaribu kulaani Israeli, na Yeye akawabariki Israeli.

207 Naam, kama Mungu huheshimu tu kanisa safi, na askofu mzuri, na mchungaji mwema sana, kundi zuri la watu walioelimika vilivyo, Yeye hana budi kukubali dhabihu hiyo, kwa sababu yeye alikuwa tu sahihi na wa kiasili kama vile Israeli walivyokuwa sahihi; bali yeye hakuwa na ufunuo wa kiroho wa Neno na mapenzi ya Mungu. Naam, hiyo ndiyo tofauti siku hizi.

208 Mtazame Yesu. Wao walisema, "Mwondoe huyu. Twajua yeye ni Msamaria. Yeye ni mwenda wazimu. Waweza kutufundisha sisi? Naam, ulizaliwa katika uzinzi. Hukuwa cho chote ila mwana haramu aliyezaliwa. Baba yako ni nani? Wasema baba yako ni Mungu, mkufuru wee! Naam, wataka kutwambia? Tumekuwa wahubiri, tumekuwa maaskofu; kupitia kwa babu zetu wa jadi wa babu wa babu wa babu wa babuwa babu wa babu zetu waliokuwa wahubiri na maaskofu. Tulizaliwa na kukuzwa kanisani. Tumepitia seminari za juu sana. Tunajua

ulisomea kila Neno barabara. Nawe unajaribu kutufundisha? Ulisomea wapi? Ulipata wapi masomo haya?"

209 Yeye alisema, "Ninyi ni wa. . .baba yenu Ibilisi," Yesu aliwaambia.

210 Hawakuwa na ishara na maajabu miogoni mwao. Hawakuwa na uponyaji wa Kiungu na kadhalika miongoni mwao. Hawakuwa na baraka miongoni mwao. Bali Yesu alikuwa ufunuo halisi wa kiroho wa Maandiko.

211 Wao walisema, "Naam, imeandikwa *hivi* na *hivi*."

212 Naye Yesu akasema, "Naam, na imeandikwa pia." Lakini Mungu alimthibitisha mtu Wake kwa ishara zake.

213 Petro alisema vivyo hivyo, katika Matendo 2, yeye alisema, "Enyi waume wa Israeli; Yesu wa Nazareti, Mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na maajabu ambayo Mungu alizifanya Kwake kati yenu, na ambazo ninyi nyote mwajua." (naam) "Aliposhikwa na. . .kwa shau. . .lile Baraza kuu la Kiyahudi pale. Bali kwa kujua kwa Mungu tangu zamani, Mungu alimchagulia tangu zamani kifo hiki. Mmemhukumu kwa mikono mikatili na miovu. Mmemsulubisha Mfalme wa Uzima, ambaye Mungu alimfufua. Nasi tu mashahidi wake."

214 Whiu, mhubiri jinsi gani! Si. . .hata hangaliweza kuandika jina lake, lakini alimjua Mungu. Walisema wao "walitambua kuwa yeye alikuwa pamoja na Yesu." Bila shaka, ni ufunuo wa kiroho. Jamani. Naam, basi.

215 Kaini alikuwa katika hali hiyo, hilo kanisa la kimwili liko hivyo siku hizi. Kanisa la Kiroho bado lingali lina ile Nguzo ya Moto, bado lina zile ishara na maajabu, lingali lina Kristo yule yule; ambaye linamthihirisha kote tangu yule mwana-kondoo aliyekufa, na katika Bustani ya Edeni, hata kule kuja kwa Mwana-Kondoo. Bila shaka, yeye yule jana, leo, na hata milele.

216 Na uzao huo wa Kaini, wa kidini, ulioerevuka na kuelimika, vivyo hivyo, ni vile vile tu, kila siku vile vile. Wakinzani na wadhalimu, kama Kaini alivyomfanyia Habili, nao ni vivyo hivyo siku hizi na wamekuwa hivyo na watakuwa hivyo; kimwili, wasioamini. Naam.

217 Sasa Mwanzo 3:8, pia niliandika 20 hapa, nimpatazama muda mchache uliopita:

> *Adamu akamwita. . .Adamu akamwita mkewe. . . Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai.* (ona, hiyo ilkuwa baada ya kudanganywa huku)

218 Kaini alikuwa. . ." Sasa ngoja! Mwasema, "Nyoka angewezaje, yule nyoka?"

219 Lakini, ndugu, tazama hapa, Biblia haisemi yeye alikuwa ni nyoka wa kawaida; Biblia ilisema, "Alikuwa mwerevu kuliko

wanyama wote wa mwitu." Yeye hakuwa anayetambaa, alikuwa mnyama. Alikuwa m...Na pale...

220 Na hebu nimpe hii kama ishara ndogo kati yetu, mkipenda. Hapo ndipo sayansi imetatanishwa kabisa. Kiumbe kinachofanana sana na mwanadamu wawezacho kupata ni sokwe. Wangapi wajua hilo? Lakini kuna kitu fulani mahali hapo. Hawawezi kuunganisha mifupa ya sokwe na ya mwanadamu, bali ndiye anayefanana naye sana. Wanaweza kumfuatilia toka kwa kiluwiluwi. Wanaweza kumfuatilia kufikia mtoto wa chura. Wanaweza kumfuatilia hata kwa mnyama na kila mnyama. Wanaweza kumfuatilia hata kwa dubu. Chukua dubu na uchune ngozi yake, anaonekana tu kama mwanamke. Kitu kile kile tu. Chukua mgongo wake na kadhalika, wasimamishe pale, na uende umvurute mwanamke kama...msimamishe mwanamke hivyo. Anafanana tu na—kama tu—kama dubu. Miguu inafanana, na mikono pia, kama tu mwanadamu. Lakini sokwe anafanana zaidi ya hivyo. Ni karibu zaidi, lakini hawawezi kuipata.

221 Hapa kuna siri mkitaka kujua. Mwajua ilipo? Imefichwa kwao. Wanaweza kuchimbua mifupa yote watakayo kuchimbua. Wanaweza kuchimbua...Mafundi wa kuchora wanaweza kuchimbua, na sayansi, na wale—wale wapima-miaka wanaweza kuipima vipimoni vya kisasa wakitumia vipimo vya atomiki, lakini hawataipata. Kwa kuwa huyo alikuwa yule nyoka aliyefanana sana na mwanadamu kuliko kitu kiwacho chote duniani, na Mungu akamlaani na kufanya atambae kwa tumbo lake, naye amegeuzwa hata akawa nyoka bila mfano wo wote wa mwanadamu. Hebu tu kwaruzeni vichwa vyenu, hawa wanasayansi, na watafakari hilo kidogo.

222 Lakini Biblia yaeleza dhahiri kuwa, "Yeye alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwituni." Naam. Yeye alikuwa ndiye kiunganisho kilichoko kati ya mwanadamu na nyani, na Mungu alimlaani na kumfanya atambae kwa tumbo lake kwa sababu ya—ya tendo lile alilolifanya. Yeye alimdaganya mwanamke huyu naye akamzaa mwanawe wa kwanza aliyekuwa Kaini (mwenye taibia za yule nyoka) kwa kutiwa pumzi; Ibilisi aliyeingia ndani ya nyoka yule, ndiye aliyefanya hayo.

223 Na ndipo Hawa akapata mimba na akazaa, akapata mimba tena baada ya kudanganywa. Sasa tazama, yeye alidanganywa, alikuwa karibu...Vema, alifanya kosa. Bali yeye bila shaka, alikuwa halali alipopata mimba kwa mumewe, kwa kuwa huenda hilo lingekuwa muda mrefu, mrefu sana baadaye, miezi mingi na siku nyingi baadaye; huwezi kujua hilo, hatujui, lakini alimzalia Adamu.

224 Na mtu fulani hata alipata lile swali, kasema, "Vema, mwana...yeye alisema Hawa ata...Na Kaini alipozaliwa, kasema, 'nimempata mtoto mwanamme kwa Bwana.'" Hakika,

bila shaka, ilibidi iwe hivyo. Ilikuwa kanuni ya viumbe. Hivyo ndivyo ulivyo hasa leo. Unapozaliwa, Mungu hashuki tu chini na kukuumba. Wewe ni mzao wa baba yako na mama yako. Na utakuwa. . .kutakuwako na. . .watoto watakuwa wazao wako. Ni kuzaana wakati wote, moja kwa moja, kama miti yenye mbegu na kadhalika; lakini kule nyuma mwanzoni. Natumai hilo lalieleza.

225 Tuna muda gani uliobakia? Hatuna. Sikiza hili zuri kwa. . . tutakalopata Jumapili; "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika mwili mmoja." Tungetaka kujua hilo. Kristo kwa wakati ule. . .Sasa, nadhani niliyapata Maandiko kadha, Maandiko mazuri kuhusu hao. [Ndugu Branham ajibu aya hii katika sehemu ya II, aya 361, kama swali la 60—Mh.]

226 Hapa kunalo hili zuri, kama tu. . .Je, mnaweza kunivumilia tu kwa dakika moja zaidi au mbili, kujibu hili? Laweza kujijibu lenyewe.

59. Unapo—unaposema, "waovu hawatateketea Milele,". . . (Vema, sasa niliwaamsha Mashahidi wa Yehova, sivyo?)**. . . Unaposema mwovu hatateketea Milele, wakusudia kuzimuni au katika lile ziwa la moto? Najua yasema katika Ufunuo** (hiyo ni sura ya 20) **kuwa kuzimu itatupwa katika lile ziwa la moto. Kama hawateketei Milele, basi itakuwaje kwao?**

227 Kama tu vile nilivyomaliza kusema, ndugu au dada, ye yote yule, wanaangamia, hawamo tena. Walikuwa na mwanzo, na pale wanakwishia; wao si kitu tena. Itakuwaje. . .watateketea kwa muda gani, hilo ni vigumu kusemwa. Lakini, tazama, kuna. . .

228 Ukiweza kupata tu hili mawazoni mwako, ona, ni rahisi sana. Kunayo tu aina moja ya Uzima wa Milele, na huo hutokana na Mungu Mwenyewe. Na Mungu pekee ndiye Uzima wa Milele. Kama utalipata tu kwa kamusi, tazama neno la Kiyunani *Zoe. Zoe* ni Uzima wa Milele." *Uzima wa Milele* ni "Mungu." Na Yesu alisema, "Nawapa Uzima wa Milele." Na ukichunguza hapa kwa kamusi, ilisema, "Zoe." Huo ndio Uzima wa Milele pekee uliopo. Hakuna mahali katika Biblia ambapo pasema kutakuwako na kuzimu kusiko na Mwanzo wala Mwisho, inasema watateketea "milele na milele."

229 Sasa pata neno "milele." Na tazama aeon—aeon. . .Je, ulitambua hapa katika Biblia? Wangapi waliwahi kusikia ikisemwa, "Na aeon na ae-. . .?" Wangapi wajua *"aeon"* ni "muda fulani"? Naam, hakika, kila mtu ajua *aeon* ni "muda fulani."

230 "Nao watachomwa kwa aeon," hiyo ni kusema muda fulani. "Watatupwa katika ziwa la moto, nao wataungua kwa aeons." *Aeon* maana yake ni "muda fulani." Huenda wakaungua kwa miaka milioni mia moja hukumuni lakini, mwishowe, hawana

budi kuangamia; kutoweka, kabisa. Ona, kwa sababu kila kitu ambacho si kikamilifu ni upotoe wa kilicho kikamilifu; na kilikuwa na mwanzo, kwa hivyo hakina budi kuwa na mwisho.

231 Bali sisi tunaoamini Bwana Yesu Kristo tuna Zoe, "Uzima wa Mungu Mwenyewe," ndani yetu, na tuna Uzima wa Milele. Si kwamba ana uzima milele na milele, mwenye dhambi ana Uzima wa milele na milele, lakini sisi tuna "Uzima wa Milele."

232 Ndugu Cox, si muda mrefu uliopita, alikuwa ameketi njiani mwangu kabla hatujaweka . . . baada kuleta ile miamba pale, na yeye akatwaa mfupa mdogo wa kale, kauliza, "Ndugu Branham, huu una umri wa miaka mingapi?"

233 "Ee," nilisema, "kwa miaka huenda ukasema una miaka elfu kumi. Aina fulani ya mnyama mdogo wa baharini wa kale aliyeishi wakati mmoja, mnyama mdogo wa baharini, huenda aliishi nyakati za kale zilizopita."

234 Yeye akasema, "Hebu waza jinsi maisha ya mwanadamu yalivyo mafupi ukilinganisha na maisha *hayo*."

235 Nikasema, "Ee lakini, ndugu, kitu hicho kina mwisho, Bali Uzima tulio nao katika Kristo hauna mwisho kile, huenda kiliishi *milele* mbili au tatu, lakini hakitakuwa kamwe na Uzima wa Milele, kwa kuwa Uzima wa Milele hutoka kwa Mungu pekee."

236 Milele, "Yeye asikiaye Maneno Yangu na kuamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Mile na hataingia hukumuni kamwe bali amepita toka mautini kuingia Uzimani." Naam, unapata Uzima wa Milele kwa kuwa mwamini. Asiyeamini ana uzima wa muda fulani. Milele . . . mwaamini ana Uzima wa Milele, na hawezi kupotea kwa sababu ni wa Milele.

237 Lakini mwamini, yeye ataenda . . . Asiyeamini atapitia ulimwenguni, atakuwa na masikitiko, laana; kile akiitacho kujumuika, "salale, kujumuika." Wanawake, mvinyo, na raha, anadhani anaendelea. Atakufa, ataenda katika ziwa la moto na viberiti linalowaka moto, ambamo moto unawaka milele na milele, na labda kwa miaka milioni mia moja nafsi yake huenda ikateseka sana katika ziwa la moto na viberiti.

238 Ni . . . Mwasema "Itakuwa tu viberiti vya kawaida?" Naamini itakuwa mara milioni nyingi kuliko hivyo. Naamini hungeweza ku . . . kuisimulia kwa moto, kwa moto wa kawaida. Sababu ya pekee ya kutumiwa "kwa moto," ni kuwa moto ndicho kitu kiteketezacho zaidi tulicho nacho. Huteketeza kabisa na kuangamiza kila kitu, moto hufanya hivyo. Vema, basi, itakuwa ndani humo, lakini utakuwa na nafsi itakayohukumiwa katika aina fulani ya . . .

239 Sasa, yakubidi uchunguze neno *moto*, kwa sababu Roho Mtakatifu limetumiwa "Roho Mtakatifu pamoja na moto," kwa

sababu moto wa Roho Mtakatifu huteketeza dhambi, ona, na husafisha.

240 Lakini moto *huu*, unatoka kuzimuni, ilisema, "ziwa la moto." Na kwa vyo vyote vile, ni adhabu yenye mateso makali. Yule tajiri aliinua macho yake, akiwa kuzimuni, na kusema, "Umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe mdomo wangu, kwa sababu ninateswa katika moto huu." Usidhani hakuna kuzimu kunakowaka moto, kuzimu halisi, kuko. Kama mna Ibilisi halisi, mna kuzimu halisi.

241 Lakini, mwaona, kila kitu kilichopotoshwa kina mwisho wake, kwa kuwa mwishowe lazima kirudie usafi huo na utakatifu wa Mungu. Na Mungu ni wa Milele, na kama tuna Uzima wa Milele, Mungu ndani yetu, hatuwezi kufa tena kuliko Mungu awezavyo kufa. Naam.

242 Sasa, kifungu kile hasa chajieleza chenyewe, ona, na kufanya dhahili. Sasa, hebu tuone, nilikuwa na . . . Sijui kama . . . Naam.

"Watakuwa—itakuwaje kwao?"

243 Wataangamia, hawako tena: ile nafsi inatoweka, roho inatoweka, uzima unatoweka, mwili unatoweka, mawazo yanatoweka, mafikira yanatoweka.

244 Na hapatakuwepo tena hata mawazo ya uovu, au yatakayokuweko ka—kamwe, Utukufuni. Naam, yote itakuwa . . . Je, waweza kuwazia, kuwa hapa wangekuwapo watu hapa katika sehemu hii . . .

245 Si Biblia husema, "Hata mawazo ya waovu yataangamia?" Hata kule kuwazia kwake kutaangamia.

246 Hapa kutakuwepo mtu *humu*, hapa yuko Mungu, Yule Mtakatifu Mkuu *hapa*, huku anajua ya kwamba kule ng'ambo mna shimo lenye nafsi zinazoteketezwa humo? Naam, hiyo haingekuwa Mbinguni. Mawazo hayo, kukumbuka huko, kila kitu kilichopotoshwa, kila wazo baya, kila kitu kitaangamia, pamoja na kila kitu kilicho kiovu ndani yake. Na hatutakuwa kitu kingine ila usafi, pamoja na *Zoe*, ule Uzima wa Mungu; hata Milele, na nyakati zitapita, na kupita na kupita na kupita na kupita; hautakwisha, itakuwa Milele!

247 "Waliingia katika adhabu ya *milele* bali wenye haki waliingia katika Uzima wa Milele." Mwafahamu? Adhabu ya *milele,* Uzima wa Milele, tofauti jinsi gani.

248 Sasa, ona, hali . . . Sasa, najua, kwenu, maskini wapendwa wangu, si—sikusudii kujionyesha mwenyewe kama mjua-yote. Nikifanya hivyo . . .

249 Sasa, nina maswali mazuri matatu au manne. Nitayajibu Jumapili asubuhi, Bwana akipenda.

250 Sasa, tazama. Ona, hili huzusha maswali. Mimi ni Mhubiri mzee. Ni—ni—ni nimekuwa hudumani miaka ishirini na sita.

Na—na—nashukuru kwake, kwamba naweza kusema hili. Si... Sijawahi kujaribu kueleza cho chote maishani mwangu kabla haijafunuliwa kwanza kwangu. Nami nashukuru sana kuwa yule Malaika wa Bwana...Huku sina elimu, sina uwezo. Na Malaika huyu alishuka, na amekuwa msaada wangu uliotumwa toka kwa Mungu. Na Yeye hajawahi kuniambia jambo moja ila lile hasa hushikamana toka Mwanzo hadi Ufunuo nalo, hata... Niliandika upesi sana Yeye aliposema, "Nawe—nawe utapeleka kipawa cha uponyaji wa Kiungu." Nami niliandika jinsi Yeye alivyoyasema.

251 Na karibu miaka mitatu baadaye, yule msimamizi akani—alinikumbusha, akisema, "Ndugu Branham, ulitambua hilo? Hilo ni kamili kabisa hata Yeye akakwambia "karama."

252 Ona, hakuwahi kusema, "ile karama." Na kila—kila moja katika Biblia...kila karama ni "ile karama," isipokuwa uponyaji wa Kiungu, na ni "karama." Ni "karama za upinyaji." Unaweza kuwa na kila aina ya karama za uponyaji, njia mbalimbali. Lakini nyingine yo yote ni "ile karama: "ile," karama ya unabii, "ile" karama ya *hii*. Lakini uponyaji wa kiungu umo katika wingi: "karama." Nami sikuwahi kuona hilo, kuwa Roho Mtakatifu ni mkamilifu sana. Ee, Bwana ahimidiwe!

253 Mwafahamu kuwa ni Roho Mtakatifu yule yule aliyeiandika Biblia, kwa kutumia mamia ya watu, ikiachana kwa mamia ya miaka...na hakuna hata mmoja wao alitofautiana na mwingine, kila mmoja wao alikuwa kamili; na hamna aliyesikia juu ya mwingine.

254 Na Paulo alikwenda kule chini, na alikuwa Arabuni, na hata hakuwa amewahi kuzuru Yerusalemu kwa miaka kumi na minne, bali alikuwa chini kule Yerusalemu na huko chini... alitoka...hakuenda kamwe Yerusalemu. Lakini kule Arabuni, na akaanza kuhubiri, hata hakuwa amemwona Petro na wengine wao kamwe kwa miaka kumi na minne. Na walipokutana, walikuwa wakihubiri mambo yale yale; ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, na uponyaji wa Kiungu katika nguvu za Mungu.

255 Ee! Nafurahi sana kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

> Mmoja wao, mmoja wao,
> Ninafurahi sana kuwa naweza kusema mimi ni
> mmoja wao; (haleluya)
> Mmoja wao, Mimi ni mmoja wao,
> Ninafurahi sana kuwa naweza kusema Mimi ni
> mmoja wao.
>
> Kuna watu karibu kila mahali,
> Ambao mioyo yao wote imewaka moto,
> Kwa moto ulioshuka Pentekoste,

Uliowasafisha na kuwafanya wasafi;
Naam, unawaka moyoni mwangu sasa,
Jina Lake litukuzwe!
Ninafurahi sana kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Walikusanyika orofani,
Wote wakiomba katika jina lake,
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Na kupata uweza kwa ajili ya huduma;
Naam, alichowatendea siku hiyo
Atakutendea vile vile,
Nina furaha sana kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Ninafurahi sana kuwa naweza kusema
Mimi ni mmoja wao: (haleluya)
Mmoja wao, mmoja wao,
Ninafurahi sana kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

256 Sikiza, ninao ujumbe mdogo kwa ajili yenu;

Njoo, ndugu yangu, tafuta baraka hii
Itakayoosha moyo wako toka dhambini,
Itakayoanzisha mlio wa kengele za furaha
Na itaiwasha nafsi yako;
Naam, inawaka moto sasa moyoni mwangu,
Ee, Jina Lake litukuzwe,
Ninafurahi sana kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

257 Je, si una furaha wewe u mmoja wao? Ni nini? Roho ndiye aliyefunua. Ni ufunuo wa Mungu, "Juu ya mwamba huu." Sijali ikiwa askofu mkuu . . .

258 Padre wa Katoliki aliketi si muda mrefu umepita, nyumbani kwangu. Naye akasema, "Bw. Branham, nilikuja kukuuliza swali."

Nilisema', "Vema bwana."

Kasema, "Nina barua hapa toka kwa askofu, yako."

Nilisema, "Vema bwana."

259 Yeye akasema, "Matamshi unayotamka, je, waweza kuuinua mkono wako na kuapa kwa uthabiti kuwa utasema kweli?"

260 Nilisema, "Sitafanya hivyo." Nilisema, "Biblia ilisema, 'Usiape kwa cho chote, kwa mbingu wala nchi (kwa kuwa ndipo pa kuwekea miguu Yake). Bali maneno yawe ndiyo, ndiyo; siyo . . . " Askofu akitaka kusikia yale nitasema, itampasa kuamini neno langu. Asipoamini, siapi."

261 Huyu padre hapa wa Sacred Heart Church, yeye akasema, "Je, ulimbatiza Paulina Frazier tarehe *fulani?"*

262 Nikasema, "nilimbatiza, bwana, katika Mto Ohio."

263 Kasema, "Ulimbatizaje?"

264 Nikasema "Nilimbatiza kwa kumtubukiza majini kwa Jina la Bwana Yesu Kristo."

265 Akaandika hayo. Kasema, "Wajua, kanisa Katoliki lilikuwa likibatiza hivyo."

Nikauliza, "Lini?"

Akasema, "Katika wakati wa mwanzoni."

Nikasema, "Wakati gani wa mwanzoni?"

Akasema, "Vema, mwanzoni."

Nilisema, "Mwanzo gani?"

Yeye akasema, "Katika Biblia."

Nilisema, "Wakusudia wale wa . . . katika—katika wanafunzi?"

Yeye alisema, "Hakika."

Nilisema, "Wawaita Katoliki wale . . . Wasema wanafunzi walikuwa Wakatoliki?"

Akasema, "Hakika, walikuwa Wakatoliki."

Nikasema, "Nilidhani kanisa Katoliki halibadiliki?"

Yeye alisema, "Halibadiliki."

266 Nikasema, "Basi mbona Petro alisema, "Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo?" Nanyi mliokuwa . . . yeye alikuwa papa?"

267 "Naam."

268 "Basi mbona mwabatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu? Na yeye alitubukiza majini, nanyi mwanyunyuzia maji. Basi imekuwaje?"

269 Yeye alisema, "Lakini, waona," kasema, "Katoliki lina mamlaka kufanya lo lote watakalo." (Ehe)

270 Nikasema "Na uliwaita wanafunzi Wakatoliki?"

271 Akasema, "Naam."

272 Nikasema, "Bwana, nina Josephus, nina *kitabu cha Fox cha Wafia Imani,* nina kitabu cha Pembeman cha *Nyakati za Mwanzoni,* nina cha Hislop, *Babeli Mbili,* historia za zamani sana silizoko ulimwenguni, nionyesha humo ambapo kanisa Katoliki liliwahi kuchaguliwa au kuwahi kufanyika dhehebu . . . miaka mia sita baada ya mtume wa mwisho."

"Ee," yeye alisema, "twaamini yale kanisa lisemayo."

Nilisema, "Naamini Biblia isimayo." Ona?

"Naam," akasema, "Mungu yuko katika kanisa Lake."

273 Nilisema, "Mungu yuko katika Neno Lake." Nami nilisema, "Kama . . . " Yeye alisema . . . Nilisema. "Biblia haisemi Mungu yuko katika kanisa Lake, lakini Biblia yasema Mungu yuko katika Neno Lake. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu; akakaa kwetu." Naam. Nilisema, "Mungu yuko katika Neno Lake."

274 Yeye alitoka nje na kusema hayo. Akasema, "Vema hatungebishana," kasema, "maana unaamini Biblia, naamini kanisa."

275 Nilisema, "Naamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu lililotiwa pumzi Yake na hakuna kuhitilafiana kwo kwote ndani Yake. Na ni Neno la Mungu, mpango Wake wa Milele kwa nyakati zote zijazo. Yeye alisema, 'Mbingu na nchi zitapita bali Neno Langu halitapita kamwe.' Naam. Naamini Neno."

276 Akamwendea mke wa Frazier. Akasema, "Bi, Frazier utaweka sahihi karatasi hii kukubali kuwa msichana wako aweza kuwa mshiriki wa kanisa Katoliki?"

277 Akasema, "Afadhali niende naye kaburini."

278 Kasema, "Huna aibu," kasema, "Yakupasa kushuhuru kuwa msichana huyo anatoka kwa upuzi huo, kuingia katika kanisa Katoliki."

279 Kasema, "Vipi kama ingekuwa msichana wako akija kanisani mwangu, ungesemaje juu ya hilo?"

280 "Ee," yeye alisema "hilo ni tofauti."

281 Kasema, "La, sivyo," Yeye alijua alikuwa mahali fulani alipomwacha maskini mwanamke huyo huko. Alijua alikuwa mahali fulani. Mama yule akasema, "Basi, mlango ule ule ulioingilia u wazi."

282 Ona, hivyo ndivyo ipasavyo usishindwe, haikupasi kushindwa. Kama Mungu yu upande wako, nani aweza kuwa juu yako? Vema! Shida ni kwamba siku hizi tuna uhafifu badala ya uthabiti. Dumu katika Mungu na katika haki!

283 Roho Mtakatifu yule yule aliyewashukia mitume na akarudi katika nyakati zilizofuata, bado yuangali Kanisani Mwake leo, wale ambao Mungu amejifunua Mwenyewe kwao. "Si katika uwezo wa yule atakaye, wala wa yule apigaye mbio, bali wa yule arehemuye, yaani Mungu." Ni Mungu, kwa kuchagua Kwake, anayewaleta watu na kufungua macho yao. Hungeweza kuliona kamwe, u kipofu, na usingeweza kuona Mungu asipofungua ufahamu wako. Biblia ilisema, u 'kipofu' na huoni. Hakuna haja ya kujaribu. Hata upate elimu ya juu jinsi gani, utaendelea tu kuwa kipofu.

284 Sasa, ninyi Church of Christ hapa, hunena pale Biblia hunena na kunyamaza inaponyamazia, na baadhi ya Haya je? Mmenyamaza kimya kabisa kuhusu Hayo. Vema.

285 Ona, inahitaji Kweli ya kiroho iliyofunuliwa. Ndipo Mungu hushuka na kujifunua Mwenyewe na kuithibitisha kuwa ni Kweli. Amina! Mnampenda? Hata nami pia. Amina.

286 Vema, ninyi Wamethodisti nyote mwataka kuamkuana kwa mkono na Wabatisti sasa? Ninyi Wapresbeteria?

287 "Naam," mwasema, "Ndugu Branham, je, wewe hukataa kushirikiana na Wabatisti na Wapresbitiria wasiobati . . . "

288 La, bwana, sifanyi hivyo. Nawachukua kuwa ndugu zangu, Hakika. Sijali kama haujabatizwa kamwe, kama ulibatizwa kwa jina la "Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Mabondeni, ile Nyota ya Asubuhi," hayo hayangekuwa . . . hiyo ingekuwa tu kama "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Vyeo vitatu tu. Yeye alikuwa Ua la Uwandani. Sivyo? Nyinyoro ya Mabondeni, ile Nyota ya Asubuhi, haya yote. Hakika, alikuwa vile. Hayo yote ni ya kitu kimoja tu, lakini jambo ni hili. Njia halisi ya Maandiko ni kwa Jina Lake Yesu Kristo. Ukitaka njia ya Kimaandiko, ndiyo hiyo hasa. Hiyo ndiyo njia halisi.

289 Sasa, kama umebatizwa katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu . . . .wajisikia kuwa hivyo ni sawa, amina. Kama ni jibu jema kwa Mungu la dhamiri safi mbele za Mungu, amina. Endelea tu, ona.

290 Bali nionavyo mimi, kwangu mimi binafsi, kama ungeliniuliza mimi, ukasema, "Ndugu Branham, yanibidi mimi nibatizwe tena?" Ningesema, "Naam," kwa upande wangu.

291 Mwanamke alikuja hapa hivi majuzi, akasema, "Bwana aliniita niwe muhubiri." Sikuamini hilo, jinsi tu nisingaliamini kuwa—kuwa yeye aweza kuruka mwezini. Naye . . .

292 Nilisema, "Vema, hilo ni zuri sana, dada." Nilisema, "Je, umeolewa?"

"Naam."

"Una watoto wawili?"

"Naam."

Nikasema, "Mu- . . . mume wako ameokoka?"

"La."

Nilisema, "Utamfanyaje?"

"Nitamwacha nyumbani."

293 Nilisema "Hicho ndicho chambo kizuri sana Ibilisi alichowahi kuwa nacho. Kwanza, wewe ni mwanamke mrembo, nawe ukitoka hapa nje hivyo hadharani kuhudumu, utakuwa chambo rahisi cha Ibilisi pamoja na shabaha yake. Na mume wako, nyumbani, kijana, na unamwachia hawa watoto wawili, yeye ataanza kutembea na mwanamke mwingine, na watoto hawa watakuwa na baba mwingine hivi karibuni." Nikasema, "Kwanza, kama Mungu angalimwita mwanamke, yeye angalitangua Neno Lake." Nikasema, "Sasa, ukitaka

kufanya hivyo, vema, basi.” Nikasema, “Sasa, utambuzi, wasema Bwana alikupa utambuzi. Je, wataka kwenda jukwaani na uujaribu?”

294 Alisema, “Naam,” Na tazama kilichotendeka.

295 Waona, ni harara. Lazima ije kwa Neno. Kama si Neno basi si sahihi. Sijali jinsi uchangamfu wako ulivyo, si sahihi. Amina! Vema, vizuri. Amina!

296 Vema:

> Tutatembea nuruni, ni nuru nzuri vipi,
> Njooni ambapo matone ya umande wa neema yanag’aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, nuru ya dunia
>
> Enyi watakatifu wote wa nuru tangazeni,
> Yesu, nuru ya dunia.
> Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
> Yesu nuru ya dunia.
>
> Tutatembea nuruni, ni nuru nzuri vipi.
> Njooni ambapo matone ya umande wa . . .
> Tuangazie kote mchana na usiku.
> Yesu nuru ya . . .

297 Sasa nataka kila mtu ageuke na aamkuane kwa mkono pande nne, na kila mtu sasa, tunapouimba huu tena;

> Tutatembea nurumi, ni nuru nzuri vipi, (Amina)
> Njooni ambapo matone ya umande wa neema yanang’aa;
> Tuangazie kote mchana ana usiku,
> Yesu, nuru ya . . .

298 Mwawapenda Wamethodisti? Semeni “Amina.” [Kusanyiko lasema “Amina—Mh.] Wabaptisti? Wapresbiteria? Wakatoliki? wa . . . Ee, mwawapenda wote? semini “Amina.” [Kusanyiko lasema “Amina”—Mh.]

> Tutatembea nuruni . . . nzu-(salimianeni, tunapoondoka)
> Ee, njoni ambapo matone ya umande wa neema yanag’aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku
> Yesu, nuru ya . . .

299 Kabla hatujaimba wimbo wetu wa kumaliza . . . Sasa, huenda ikawa nitakuwa hapa tena Jumapili. Sasa, baada ya hapo sitakuwepo tena hadi baada ya sikukuu. Ona, kwa kuwa naenda Michigan, toka Michigan hadi Colorado, toka Colorado hadi kule Idaho, toka Idaho hadi kule Califonia, kisha tutarudi. Na inawezekana (nawatakeni mniombee). Nitakuwa Waterloo, Iowa, mwanzoni mwa Januari ishirini na nne hadi Februari

mbili. Ona, huo uwanja mkubwa pale, nilipata simu muda mchache uliopita, na nina tangu sasa hata Jumapili kuomba. Ona, kule Waterloo, Iowa, ambapo ni karibu sasa.

300 Lakini sasa, kumbuka, sikizeni kipindi cha redioni cha ndugu saa tatu asubuhi, Jumamosi asubuhi, tutampigia simu na kumjulisha. Na kitawajia toka kwa WLRP, kwaya ya watu wanne ya Neville saa tatu asubuhi, Jumamosi asubuhi. Tuta . . . kama si—sitayafikia, Ndugu Neville atayamaliza maswali haya. Je, Ndugu Neville utafanya hivyo, Jumapili asubuhi? [Ndugu Neville acheka na kusema, "Kazi kubwa"—Mh.] Vema, tazama, ukipata shida, nitakusaidia. Yeye ataona. Vema,

301 Vema:

> Peleka jina la Yesu,
> Po pote uendako;
> Litafurahisha moyo
> Peleka uendako.
>
> Dhamani na tamu,
> Ni jina lake Yesu;
> Dhamani (dhamani) na tamu, (na tamu)
> Ni jina lake Yesu;

302 Sasa, mkitaka kumjua mbaptisti anayeamini kupiga shangwe, huko ndiko kushangilia ninakoamini. Huyo mama mkongwe aliyeketi pale, na Roho akamjia. Alianza kulia, hangejizuia, akarudi nyuma na kumbusu binti yake. Hivyo ndivyo nipendavvo kuiona. Amina. Hilo ni nzuri kabisa, ya mtindo wa kale, upendo unaogusa moyo. Jamani mtakatifu m—mkogwe, aliyekolea, aliyekomaa, aliye tayari kwenda nyumbani utukufuni. Anangojea tu kuitwa, mwaona, mwenye furaha tele.

Vema, Ndugu Neville sasa, cho chote anachotaka kutenda.

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org